UTANGULIZI

Mkataba wa Umoja wa Mataifa ulitiwa sahihi tarehe 26 Juni mwaka 1945, katika mji wa San Fransisco, mwishoni mwa mkutano wa Umoja wa Mataifa, juu ya Shirika la Ulimwengu, na ulianza kutumika tarehe 24 Octoba mwaka 1945. Sheria ya Mahakama ya Mataifa pia ni sehemu ya Mkataba huo.

Mabadiliko ya sehemu za 23, 27 na 61 za Mkataba huo, yalikubaliwa na Baraza Kuu tarehe 17 Desemba 1963 na kuanza kutumiwa mwaka 1965 tarehe 31 Agosti. Sehemu ya 109 ya Mkataba huo ilibadilishwa na kukubaliwa na Baraza Kuu tarehe 20 Desemba mwaka 1965, na kuanza kutumika tarehe12 Juni 1968.

Badiliko la sehemu ya 23 ya Mkataba huo linazidisha idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Usalama kutoka kumi na moja, na kuwa kumi na tano. Mabadiliko ya sehemu ya 27 yanataraji uthibitisho wa azimio litakalopitishwa na Halmashauri hiyo, lipate wingi wa kura tisa, badala ya saba kama ilivyokuwa awali, na maazimio mengine ya jumla pia yatahitaji kupata kura tisa, badala ya saba za zamani, pamoja na kura za wajumbe wa kudumu katika Halmashauri hiyo.

Badiliko la sehemu ya 61 ambalo lilianza kutumika tarehe 31 Agosti 1965 linazidisha idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Uchumi na Ustawi wa Jamii kuwa wajumbe ishirini na saba badala ya kumi na nane ilivyokuwa awali. Badiliko hilo ambalo lilianza kutumika tarehe

24 Septemba 1973 pia linaongeza wajumbe wa Halmashauri hiyo kutoka ishirini na saba mpaka hamsini na nne.

Badiliko la sehemu ya 109, linahusu kifungu cha kwanza cha sehemu hiyo kinachoeleza juu ya Mkutano Mkuu wa Nchi za Umoja wa Mataifa ili kufikiria tena Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ambao ungeweza kufanywa wapi, na tarehe gani, kwa kupata idhini ya kura theluthi mbili za wajumbe wa Baraza Kuu, na kura za wajumbe tisa wa Halmashauri ya Usalama badala ya wajumbe saba kama ilivyokuwa awali. Kifungu cha tatu cha sehemu hiyo ya 109, kimeachwa kama kilivyokuwa, kuhusu kufikiria mkutano wa kawaida kila baada ya kukutana mara kumi kwa Baraza Kuu. Kadhalika kwa kufuata kanuni ile ile ya "kura saba za Wajumbe wa Halmashauri ya Usalama". Kifungu hicho kilijadiliwa na Baraza Kuu mwaka 1955, wakati wa kikao chake cha kawaida cha kumi, kadhalika na Halmashauri ya Usalama.

KATIBA YA UMOJA WA MATAIFA

SISI WATU WA UMOJA WA MATAIFA TUMEAZIMIA

kuokowa vizazi vya siku za mbele na misiba ya vita ambavyo katika maisha yetu vimewaletea wanadamu huzuni zisizosemeka mara mbili, na

kuzidi kuthibitisha imani katika haki za lazima za binadamu, katika ubora na ustahiki wa mwanadamu, katika usawa na haki baina ya wanaume na wanawake na baina ya mataifa makubwa na madogo, na

kuweka masharti ambayo yatahakikisha kufuatwa haki na kutukuzwa yale yapasayo katika mikataba na mambo mengineo yanayohusu sheria za mataifa, na

kuzidisha maendeleo ya watu na kutengeneza hali za maisha katika hali kubwa zaidi ya uhuru,

NA KWA KUYAFIKILIA HAYA

kuvumilia na kuishi pamoja kwa salama baina yetu kama majirani wema, na

kuunganisha nguvu zetu ili kuhifadhi salama na amani baina ya mataifa, na

kuhakikisha, kwa kuikubali misingi na uanzishaji wa taratibu iliyomo, kuwa nguvu za silaha hazitotumiwa ila kwa manufaa ya watu wote, na

kutumia madaraka ya mataifa kwa kuendeleza uchumi na maendeleo ya watu wote.

TUMEAZIMIA KUUNGANISHA BIDII ZETU ILI KUYAFIKILIA MAAZIMIO HAYA

Kwa hivyo Serikali zetu ambazo manaibu wake walikutana katika mji wa San Fransisco na ambao walionyesha hati zao zilizoonekana kuwa zimekamilika wameukubali Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa na wamekianzisha chama cha mataifa kinachoitwa Umoja wa Mataifa.

SURA YA 1

MADHUMUNI NA KAWAIDA

Sehemu ya 1

Madhumuni ya Umoja wa Mataifa ni:—

1. Kuhifadhi salama na amani baina ya mataifa, na kuyafikilia haya: kuchukua kwa pamoja hatua kamili za kuzuia na kuondosha vitisho vya kuondoa amani na kukomesha vitendo vya shari au vya kuvunja amani, na kuleta kwa njia ya salama na kwa kulingana na misingi ya haki na sheria za mataifa, matengenezo au mapatanisho ya matatizo ya mataifa au mambo ambayo huenda yakaondoa salama.

2. Kusitawisha urafiki baina ya mataifa na kuiheshimu misingi ya usawa wa haki baina ya watu na watu kuchagua watakalo wenyewe, na kuchukua hatua nyinginezo zinazofaa kuimarisha salama ya dunia.

3. Kupata ushirikiano wa mataifa katika kutafuta njia za kuondoa matatizo ya mataifa yanayohusu uchumi, mambo ya starehe, utamaduni au tabia za binadamu, na kushirikiana katika kuleta na kuhimiza kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa lazima kwa wote bila ya kubaguzi wa kabila, mwanamume au mwanamke, lugha au dini, na

4. Kuwa ni makao ya kulinganisha vitendo vya mataifa ili kuyafikilia madhumuni haya ya wote.

Sehemu ya 2

Katika kuendeleza madhumuni yaliyotajwa katika Sehemu 1, chama hiki na wanachama wake watafuata misingi ifuatayo:—

1. Chama hiki kinategemea msingi wa usawa wa utawala kwa wanachama wake wote.

2. Ili kuwahakikishia wote, haki na faida zitakazopatikana kwa kuwa mwanachama, wanachama wote watatekeleza wajibu wao waliojichukulia kwa mujibu wa hati hii.

3. Wanachama wote watapatana juu ya ugomvi wa mataifa yao kwa njia za salama ambazo hazitatia hatarini amani, salama ya mataifa na haki.

4. Wanachama wote watajizuia, katika uhusiano wao na mataifa mengineo, na kutumia vitisho au nguvu juu ya usalama wa nchi au uhuru wa siasa ya nchi yo yote, au kutumia njia ye yote nyingineyo kinyume cha madhumuni ya Umoja wa Mataifa.

5. Wanachama wote wataupa Umoja wa Mataifa kila msaada katika jambo lo lote utakalolifanya kwa mujibu wa Mkataba huu, na watajizuia kutoa msaada kwa dola ye yote

ambao Umoja wa Mataifa unachukua hatua ya kuzuilia au kuilazimisha jambo.

6. Chama hiki kitahakikisha kwamba dola ambazo si wanachama wa Umoja wa Mataifa zitafata kawaida hizi kama itakavyolazimika ili ipatikane amani na salama baina ya mataifa.

7. Hapana katika yaliyomo ndani ya hati hii litakaloupa Umoja wa Mataifa ruhusa ya kuingilia mambo yanayohusu utawala wa ndani wa dola ye yote au kuwataka wanachama kupeleka mambo kama hayo kwenye mapatanisho kwa mujibu wa Mkataba huu; lakini kawaida hii haitaharibu utumiaji wa hatua za kutia nguvu zilizoelezwa katika Sura ya VII

SURA YA II

UWANACHAMA

Sehemu ya 3

Wanachama wa asili wa Umoja wa Mataifa ni zile dola ambazo baada ya kushirikiana katika mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Shirika la Ulimwengu uliokuwepo San Fransisco, au zile dola ambazo ziliwasili kuitia sahihi ile taarifa ya Umoja wa Mataifa ya mwezi 1 January, 1942, wametia sahihi Mkataba huu na kuuthibitisha kwa mujibu wa sehemu ya 110.

Sehemu ya 4

1. Kuwa mwanachama katika Umoja wa Mataifa kunawezekana kwa dola zote nyinginezo zinazopenda salama ambazo zitayakubali yale mambo yanayopaswa kufanywa yaliyokuwamo katika Mkataba huu na ambazo katika maoni ya chama zinaweza na ni tayari kuyafuata mambo hayo.

2. Kukubaliwa kwa nchi yo yote kama hiyo kuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa kutategemea shauri litakalokatwa na Baraza Kuu baada ya kulizingatia pendekezo la Baraza la Usalama.

Sehemu ya 5

Mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambaye Baraza la Usalama limechukuwa hatuwa ya uzuwizi au ya kutilia nguvu jambo juu yake huenda akazuiliwa kutumia haki na nafuu zake za uanachama na Baraza Kuu baada ya kulizingatia pendekezo la Baraza la Usalama. Kutumia haki na nafuu hizi zaweza kurejeshwa na Baraza la Usalama.

Sehemu ya 6

Mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambaye atashikilia kuivunja misingi ya Mkataba huu aweza kutolewa katika chama na Baraza Kuu baada ya kulizingatia pendekezo la Baraza la Usalama.

SURA YA III

SEHEMU KUU

Sehemu ya 7

1. Zifuatazo ni sehemu kuu za Umoja wa Mataifa; Baraza Kuu, Baraza la Usalama, Baraza la Uchumi na mambo ya Starehe, Baraza la Udhamini, Mahakama ya Ulimwengu na Idara ya Katibu.

2. Sehemu nyingine ndogo ambayo huenda ikawa lazima kuwepo yaweza kufunguliwa kwa mujibu wa Mkataba huu.

Sehemu ya 8

Umoja wa Mataifa hautoweka pingamizi yo yote katika kuwakubali wanaume na wanawake kushika cheo cho chote kile na kuwa na hali za usawa katika sehemu zake kuu na ndogo.

SURA YA IV

BARAZA KUU

MJENGO

Sehemu ya 9

1. Baraza Kuu litakuwa na wanachama wote wa Umoja wa Mataifa.

2. Kila mwanachama hatoweza kuwa na Wajumbe zaidi ya watano katika Baraza Kuu.

KAZI ZAKE NA UWEZO WAKE

Sehemu ya 10

Baraza Kuu linaweza kuzungumza jambo lolote au mambo yo yote yanayoingia katika Mkataba huu au yanayohusu uwezo na kazi za sehemu yo yote iliokuwemo katika Mkataba huu na, linaweza kupeleka mapendekezo yake mbele ya wanachama wa Umoja wa Mataifa au mbele ya Baraza la Usalama au kote kuwili juu ya jambo lolote hilo au mambo yo yote hayo isipokuwa kama ni kwa kufuata namna ile iliyotajwa katika Sehemu ya 12.

Sehemu ya 11

1. Baraza Kuu laweza kufikiria misingi ya kushirikiana katika kuhifadhi amani na Usalama wa Ulimwengu na vile vile misingi ya kupunguza silaha za mataifa na kuzingatia utumizi wa silaha za vita, na linaweza kupeleka mapendekezo yake mbele ya wanachama au mbele ya Baraza la Usalama au mbele ya kote kuwili.

2. Baraza Kuu linaweza kuzungumza juu ya jambo lolote linalohusu kuhifadhi amani na usalama wa ulimwengu ambalo limepelekwa mbele yake na Mwanachama wa Umoja wa Mataifa au na Baraza la Usalama, au na nchi ambayo si mwanachama wa Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa sehemu ya 35, fasili ya 2 na, isipokuwa kwa namna iliyotajwa katika

sehemu ya 12, linaweza kupeleka mapendekezo yake juu ya jambo lolote la namna hiyo kwa nchi hiyo au nchi hizo zilizohusika au kupeleka kwa Baraza la Usalama au kupeleka kote kuwili. Baraza Kuu litapeleka jambo lolote la namna hiyo, ambalo itabidi kuchukuliwa hatua juu yake, mbele ya Baraza la Usalama kabla au baada ya kulizungumza.

3. Baraza Kuu laweza kulizindusha Baraza la Usalama juu ya hali ambazo zinaweza kutia hatarini amani na salama baina ya mataifa.

4. Uwezo wa Baraza Kuu uliowekwa katika sehemu hii hautokuwa kizuizi juu ya yaliyoelezwa katika sehemu ya 10.

Sehemu ya 12

1. Itakapokuwa Baraza la Usalama linafanya kazi kwa mujibu wa Mkataba huu juu ya tatizo lo lote au hali yo yote, Baraza Kuu halitopeleka mapendekezo yo yote juu ya tatizo hilo au hali hiyo ila ikiwa Baraza la Usalama litataka hivyo.

2. Katibu Mkuu kwa ruhusa ya Baraza la Usalama atalipasha habari Baraza Kuu katika kila mkutano juu ya mambo yo yote yanayohusu hifadhi ya amani na salama ya ulimwengu ambayo yanashughulikiwa na Baraza la Usalama. Katibu Mkuu vile vile atalipa habari Baraza Kuu, au ikiwa Baraza Kuu halina mkutano, atawapa habari wanachama wa Umoja

wa Mataifa mara tu Baraza la Usalama litakapoacha kushughulika na mambo hayo.

Sehemu ya 13

1. Baraza Kuu litaanzisha mafunzo na kutoa mapendekezo kwa madhumuni ya:—

(a) kuendeleza ushirikiano wa mataifa katika mambo ya siasa na kutilia nguvu maendeleo ya kukuza sheria ya mataifa na kuweka taratibu za sheria.

(b) Kuendelea ushirikiano wa Mataifa katika mambo ya uchumi, ya starehe, utamaduni, elimu na afya, na kusaidia katika kutambulikana haki za binadamu na misingi ya uhuru kwa watu wote bila ya kubagua kabila, mwanamume au mwanamke lugha au dini.

2. Madaraka zaidi, kazi na uwezo wa Baraza Kuu katika mambo yaliyotajwa katika fungu la 1(6) hapo juu yametajwa katika Sura ya IX na X.

Sehemu ya 14

Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya 12, Baraza Kuu laweza kupendekeza hatua za kuchukuliwa kwa mapatanisho ya amani juu ya matatizo yoyote, bila kuangalia mwanzo wake, ambayo Baraza Kuu linayafikiria kuharibu hali njema au kuharibu uhusiano

wa urafiki baina ya mataifa, pamoja na matatizo yatokanayo na kuvunjwa masharti yaliyomo katika Mkataba uliopo ambayo yanaeleza madhumuni na kawaida za Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 15

Baraza Kuu litapokea na kuzingatia ripoti za mwaka na ripoti maalum zitokazo Baraza la Usalama, ripoti hizi zitakuwa na maelezo ya mambo ambayo Baraza la Usalama limeyaazimia au limeyafanya ili kuhifadhi salama na kuondoa hofua ina ya mataifa.

2. Baraza Kuu litapokea na kuzingatia ripoti kutoka sehemu nyinginezo za Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 16

Baraza Kuu litafanya zile kazi zinazohusu mpango wa udhamini wa mataifa ambazo Baraza Kuu limepewa kuzifanya kwa mujibu wa Sura ya XII na XIII, pamoja na kuikubali mikataba ya udhamini kwa mahala pasipochaguliwa kuwa ni muhimu kwa mambo ya vita.

Sehemu ya 17

1. Baraza Kuu litaizingatia na kuikubali hesabu ya Chama inayohusu matumizi na mapato.

2. Gharama za chama zitalipwa na wanachama kama litakavyogawa Baraza Kuu.

3. Baraza Kuu litazingatia na kuikubali mipango yo yote ya pesa au inayohusu matumizi na mapato pamoja na wakala maalum zilizotajwa katika sehemu ya 57 na itaichungua mipango ya ndani ya pesa ya hizo wakala maalum kwa madhumuni ya kuzipelekea wakala hizo mapendekezo ya Baraza Kuu.

Kupiga kura:

Sehemu ya 18

1. Kila mwanachama wa Baraza Kuu atakuwa na kura moja.

2. Baraza Kuu litatoa uamuzi wake juu ya mambo muhimu kwa kupatikana kura ya theluthi mbili za wanachama watakaohudhuria mkutano na watakaopiga kura. Mambo hayo ya mataifa na amani, uchaguzi wa wanachama wasiokuwa wa daima wa Baraza la Usalama, uchaguzi wa wanachama wa Baraza la Uchumi na mambo ya starehe, uchaguzi wa wanachama wa Baraza la Udhamini kwa mujibu wa fasili 1(c) ya sehemu ya 86, kupokelewa wanachama wapya katika Umoja wa Mataifa, kuzuiliwa haki na nafuu za uwanachama, kufukuzwa kwa wanachama, mambo yanayohusu maendeleo ya mpango wa udhamini na mambo yanayohusu matumizi na mapato.

3. Shauri juu ya mambo mengine, pamoja na maazimio ya kuongeza mambo mengineo ya kukatiwa shauri kwa kupatikana wingi wa theluthi mbili za kura yatakatwa kwa kupatikana kura nyingi kwa wanachama wataohudhuria mkutano na watakaotoa kura zao.

Sehemu ya 19

Mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambaye anadaiwa na Umoja huu mchango wake wa pesa hatokua na kura katika Baraza Kuu ikiwa kiasi anachodaiwa ni sawa au zaidi ya jumla ya mchango wake kwa miaka miwili kamili iliyopita Juu ya hayo Baraza Kuu linaweza kumuachia mwanachama huyo kutoa kura yake ikiwa limetoshelezeka kuwa kutokulipwa mchango kumesababishwa na mambo ambayo huyo mwanachama hana nguvu nayo.

Taratibu:

Sehemu ya 20

Baraza Kuu litakutana mikutano ya dasturi kwa kila mwaka na mikutano maalum kama itakavyohitajikana. Mikutano maalum itaitwa na Katibu Mkuu kutokana na maombi ya Baraza la Usalama au ya wanachama wataozidi nusu ya wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 21

Baraza Kuu litatengeneza kanuni zake za taratibu yake, Baraza Kuu litamchagua Rais kwa kila mkutano.

Sehemu ya 22

Baraza Kuu linaweza kufungua sehemu ndogo ndogo kama itavyolazimika kwa kuendesha kazi zake.

SURA YA V

HALMASHAURI YA USALAMA

Sehemu ya 23

1. Halmashauri ya Usalama itakuwa na wanachama kumi na tano wa Umoja wa Mataifa, Urusi, Jamhuri ya China, Ufaransa, Umoja wa Ulaya ya Kiingereza na Ireland ya Kaskazini, na Umoja wa nchi za Amerika zitakuwa wanachama wa daima wa Baraza la Usalama. Baraza Kuu litachagua wajumbe wengine kumi na Umoja wa Mataifa, kuwa wajumbe wa muda katika Halmashauri au Baraza la Usalama, katika kuhifadhi usalama na amani ya mataifa na mambo mengine katika madhumuni ya Umoja, na vilevile

utatazamwa udhaifu wa mgawanyiko kwa mujibu wa jiografia.

2. Wanachama wasio wa daima wa Baraza la Usalama watachaguliwa na kukaa kwa muda wa miaka miwili. Zaidi ya hivyo katika uchaguzi wa mwanzo wa wanachama wasio wa daima wanachama wawili katika idadi ya wanne zaidi watachaguliwa kushika madaraka ya uanachama wa mwaka mmoja, kutokana na kuzidishwa kwa idadi ya wajumbe wa Baraza la Usalama kutoka wajumbe kumi na moja mpaka kumi na tano. Mjumbe atakayechaguliwa hivyo anaweza kuchaguliwa tena, mara tu baada ya muda wake kumalizika.

3. Kila nchi iliyochaguliwa kuwakilishwa katika Halmashauri ya Usalama, itakuwa na mjumbe wake mmoja tu.

Kazi yake na uwezo wake

Sehemu ya 24

1. Kwa kuhakikisha kuwa Umoja wa Mataifa utafanya kazi kwa upesi na kupatikana lililokusudiwa, wanachama wake wanalipa Baraza la Usalama madaraka ya kuhifadhi salama na amani ya mataifa na wanakubali kuwa katika kuzifanya kazi zake kwa mujibu wa madaraka haya Baraza la Usalama litakuwa inafanya kazi kwa niaba yao.

2. Katika kuifanya kazi hii Baraza la

Usalama litafuata madhumuni na misingi ya Umoja wa Mataifa. Nguvu halisi zilizopewa Baraza la Usalama kwa kuzifanya kazi hizi zimo katika Sura za VI, VII, VIII na XII.

3. Baraza la Usalama litapeleka mbele ya Baraza Kuu kwa kuzingatiwa ripoti za mwaka na itapokuwa lazima, ripoti maalum.

Sehemu ya 25

Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanakubaliana kukubali na kufuata uamuzi wa Baraza la Usalama kwa mujibu wa Mkataba huu.

Sehemu ya 26

Ili kuendeleza kuwepo na kuhifadhiwa salama na amani ya mataifa kwa utumizi mchache itakavyowezekana wa silaha za kibinadamu na za Uchumi wa Ulimwengu, Baraza la Usalama litakuwa ni kazi yake kutengeneza, kwa msaada wa Halmashauri ya jeshi la kiaskari iliyotajwa katika sehemu ya 47, mipango ya kuleta njia ya kurekebisha silaha na kupeleka mbele ya wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Kupiga kura:

Sehemu ya 27

1. Kila mjumbe wa Baraza la Usalama atakuwa na haki ya kupiga kura moja.

2. Uamuzi wa Baraza la Usalama juu ya shughuli zake za kawaida, utapitishwa kwa wingi wa kura tisa, za wajumbe wake.

3. Uamuzi wa Baraza la Usalama juu ya mambo mengine yote, utapitishwa kwa kura za wajumbe tisa pamoja na wajumbe wa kudumu, isipokuwa tu kwa kufuata kifungu cha tatu cha sehemu ya 52 mjumbe wa nchi ambayo inahusika na suala linalojadiliwa na Baraza hilo hatakuwa na haki ya kupiga kura, kama ilivyokwisha kubaliwa katika Sura ya VI ya Mkataba ya Umoja wa Mataifa.

Taratibu:

Sehemu ya 28

1. Baraza la Usalama litapangwa kwa maana ambayo litaweza kufanya kazi bila ya kusita. Kwa madhumuni haya kila mwanachama wa Baraza la Usalama atakuwa na mjumbe wake katika kikao cha Baraza Kuu.

2. Baraza la Usalama litafanya mikutano kila baada ya muda maalumu na katika mikutano hiyo kila mwanachama ikiwa atataka, anaweza kushikiwa pahala pake na mwanachama wa serikali yake au na naibu maalumu mwengineo.

3. Baraza la Usalama linaweza kufanya mikutano mahali po pote mbali na kikao cha

Umoja wa Mataifa ikiwa litaona kuwa kazi yakeitafanyika kwa wepesi kabisa.

Sehemu ya 29

Baraza la usalama linaweza kufungua sehemu ndogo ndogo kama itavyolazimika kwa kufanya kazi zake.

Sehemu ya 30

Baraza la Usalama litatengeneza kanuni zake za taratibu yake pamoja na namna ya kumchagua Rais wake.

Sehemu ya 31

Mwanachama yo yote wa Umoja wa Mataifa ambaye si mwanachama wa Baraza la Usalama anaweza kuwemo bila ya kuweza kupiga kura, katika mazungumzo juu ya jambo lo lote litakaloletwa mbele ya Baraza la Usalama litakapoona Baraza la Usalama kuwa jambo hilo laingilia masilahi ya mwanachama huyo.

Sehemu ya 32

Mwanachama yo yote wa Umoja wa Mataifa ambaye si mwanachama wa Baraza la Usalama au nchi yo yote ambayo si Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, ikiwa ni mdaawa katika ubishi unaofikiriwa na Baraza la Usalama, itaitwa iwemo katika mazungumzo ya ugomvi huo bila ya kuweza kupiga kura yake. Baraza la Usalama litaweka shuruti kama itakavyoona zinafaa kwa kuwemo katika mazungumzo nchi ambayo si Mwanachama wa Umoja wa Mataifa.

SURA YA VI

KUAMUA UGOMVI KWA SALAMA

Sehemu ya 33

1. Watakaokuwamo katika ugomvi ambao ukiendelea umeelekea kutia hatarini kuwepo kwa salama na amani ya mataifa, kwanza watajaribu kusikilizana kwa mapatano, kufanya uchunguzi, kufanya suluhu, kuafikiana, kupeleka ugomvi mbele ya mwamuzi, suluhu ya mahakama, kuwarudia mawakala wa nchi au mpango ya nchi, au kwa njia yo yote nyingineo ya usalama watakaochagua.

2. Itakapoona ni lazima, Baraza la Usalama litawataka hao wataokuwemo ugomvini wapatane kwa njia kama hizo.

Sehemu ya 34

Baraza la Usalama linaweza kuchungua ugomvi wo wote au hali yo yote ambayo itaweza kuleta mabishano baina ya mataifa au ambayo itaweza kuleta ugomvi ili kuhakikisha kama kuendelea kwa ugomvi huo au hali hiyo kumeelekea kuitia hatarini hali ya kuweko salama na amani ya mataifa.

Sehemu ya 35

1. Mwanachama yo yote wa Umoja wa

Mataifa anaweza kupeleka ugomvi wo wote au hali yo yote ya namna iliyotajwa katika sehemu ya 34 mbele ya Barazala Usalama au mbele ya Baraza Kuu.

2. Nchi ambayo si mwanachama wa Umoja wa Mataifa inaweza kupeleka mbele ya Baraza la Usalama au mbele ya Baraza Kuu ugomvi wo wote ambao hiyo nchi imehusikana nao ikiwa hiyo nchi mbele itazikubali, kwa madhumuni ya ugomvi huo, shuruti za uamuzi wa salama zilizotajwa katika Mkataba huu.

3. Mashauri ya Baraza Kuu juu ya mambo yaliyopelekwa mbele yake kwa mujibu wa sehemu hii yatabidi kufuata masharti ya Sehemu ya 11 na 12.

Sehemu ya 36

1. Baraza la Usalama wakati wo wote itakapokuwa ugomvi wa namna iliyotajwa katika sehemu ya 33 unaendelea au hali ya namna hiyo inaendelea, linaweza kutoa mapendekezo juu ya taratibu inayofaa au njia za kusawazisha mambo.

2, Baraza la Usalama litabidi kuzingatia mipango yo yote ya kupatana ugomvi ambayo wenye kugombana wameshaichagua.

3. Katika kutoa mapendekezo kwa mujibu wa Sehemu hii Baraza la Usalama litabidi vile vile kuzingatia kuwa ugomvi unaohusu

mambo ya sheria utabidi kwa desturi upelekwe na wenye kugombana mbele ya Mahakama ya Mataifa kwa Mujibu wa Sheria ya Mahakama.

Sehemu ya 37

1. Ikiwa wenye kugombana ugomvi wa namna uliotajwa katika sehemu ya 33 wata shindwa kusikilizana kwa njia zilizoelezwa katika sehemu hiyo, itawabidi kupeleka ugomvi wao mbele ya Baraza la Usalama.

2. Ikiwa Baraza la Usalama litaona kuwa kuendelea kwa ugomvi kwa hakika kumeelekea kuitia hatarini hali ya kuwepo salama na amani ya mataifa, litakata shauri ama kutenda kwa mujibu wa sehemu ya 36 au kutoa mapendekezo juu ya namna za mapatano kama litakavyoona kuwa ndivyo.

Sehemu ya 38

Bila ya kuharibu yaliyomo katika sehemu ya 33 mpaka ya 37, Baraza la Usalama, ikiwa wote wenye ugomvi watataka, litaweza kuwapa nasaha wenye ugomvi ili kuleta mapatano ya salama.

SURA YA VII

MAMBO YA KUFANYA VITAKAPOKUWEKO VITISHO VYA KUONDOA AMANI, AU VITAKAPOTENDEKA VITENDO VYA KUONDOA SALAMA NA VYA UADUI

Sehemu ya 39

Baraza la Usalama litakata maneno juu ya kuweko vitisho vya kuondoa amani, kutendeka vitendo vya kuondoa salama au vya uadui, au litakata shauri juu ya mambo ya kufanywa kwa mujibu wa sehemu ya 41 na 42, ili kuhifadhi au kurejesha salama na amani ya mataifa.

Sehemu ya 40

Ili kuyazuia mambo yasizidi kuharibika, Baraza la Usalama, kabla ya kutoa mapendekezo yake au kukata shauri juu ya mambo ya kufanya kwa mujibu wa sehemu ya 39, linaweza kuwataka wale wenye ugomvi kufuata kwa muda fulani mipango maalumu itakayoiona lazima au yenye manufaa. Mipango hiyo ya kufuatwa kwa muda fulani haitaharibu haki, madai au hali ya wenye ugomvi. Baraza la Usalama litazingatia ipasavyo kuacha kufuatwa hiyo mipango maalumu ya kufuatwa kwa muda fulani.

Sehemu ya 41

Baraza la Usalama linaweza kutaka shauri juu ya mipango ya kufuatwa ili kutimiza uamuzi wake na ambayo isiyohitajia kutumika nguvu za silaha, na linaweza kuwataka wanachama wa Umoja wa Mataifa waifuate mipango hiyo. Mipango yenyewe yaweza kuwa kukatwa kabisa au sehemu ya uhusiano wa uchumi na wa reli, bahari, hewa, posta, simu, radio na njia nyinginezo na kuondosha uhusiano wa baina ya mataifa.

Sehemu ya 42

Ikiwa baraza la Usalama litaona kuwa mipango iliyowekwa katika sehemu ya 41 itakuwa si ya kutosha au imeonyesha kuwa si ya kutosha, basi linaweza kuchukua hatua ya kutumia nguvu za hewani, baharini au za nchi kavu kama itavyolazimika ili kuwezesha kuwepo au kuirudisha hali ya salama na amani baina ya mataifa. Hatua hiyo inaweza kuwa ya maonyesho, mazingira na mipango mingineo ya kutumia nguvu za hewani, baharini au za nchi kavu za wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 43

1. Ili kuwezesha kuwepo salama na amani baina ya mataifa, wanachama wote wa Umoja wa Mataifa wanaahidi kuweka tayari kwa matumizi ya Baraza la Usalama litapohitajia

na kwa mujibu wa mapatano maalumu, nguvu za silaha, msaada na njia za kuwezesha mambo kutendeka kwa wepesi pamoja na haki za kutumia njia, ambayo ni lazima kwa kuihifadhi salama na amani baina ya mataifa.

2. Mapatano hayo yataeleza idadi na namna ya hizo nguvu, uwezo wake wa kuwa tayari na mahala zitakapokuweko, na itaeleza namna ya hizo njia za kuwezesha mambo kutendeka kwa wepesi na namna ya msaada utakaotolewa.

3. Mapatano yatatengenezwa kwa upesi kama itavyomkinika kwa kutiliwa nguvu na Baraza la Usalama. Mapatano hayo yatakuwa baina ya Baraza la Usalama na wanachama au baina ya Baraza la Usalama na vifungu vya wanachama na yatakuwa yenye kuweza kuthibitishwa na nchi zitakazotia sahihi kwa mujibu wa mpango ya kanuni za katiba za serikali za kila nchi.

Sehemu ya 44

Litakapokata shauri Baraza la Usalama kutumia nguvu, na kabla ya kumtaka mwanachama asiyekuwemo katika Baraza hilo kutoa nguvu za silaha kwa kutekeleza wajibu ulio jichukulia katika sehemu ya 43, litamkaribisha mwanachama huyo, ikiwa atataka awemo katika mashauriano ya Baraza la Usalama yanayohusu kutumika kwa vikosi vya askari na silaha za mwanachama huyo.

Sehemu ya 45

Ili kuuwezesha Umoja wa Mataifa kuchukua hatua ya hivi kwa upesi, wanachama watakuwa na vikosi vya mataifa yao vya wanahewa vitakavyoweza kutumika kwa haraka kwa hatua ya kushirikiana badala ya kutumia nguvu. Nguvu na hali ya kuwa tayari ya vikosi hivi na mipango ya kitendo chao cha shirika itawekwa na Baraza la Usalama kwa msaada wa halmashauri ya mambo ya vita kwa kufuata namna iliyowekwa katika mapatano maalumu yaliyotajwa katika sehemu ya 43.

Sehemu ya 46

Mipango ya kutumia nguvu za silaha itatengenezwa na Baraza la Usalama kwa msaada wa Halmashauri ya mambo ya vita.

Sehemu ya 47

1. Kutachaguliwa halmashauri ya mambo ya vita ili kulipa shauri na kulisaidia Baraza la Usalama juu ya mambo yote ya Baraza la Usalama yanayohusu mahitajio ya vita ili kuhifadhi salama na amani baina ya mataifa, na juu ya kutumia majeshi yaliyowekwa chini yake na namna ya kuyaamuru majeshi hayo, juu ya kudhibiti zana za vita na uwezekano wa kuacha silaha.

2. Watakuwemo katika halmashauri ya mambo ya vitani wakuu wa wanachama wa

daima wa Baraza la Usalama au manaibu wao. Mwanachama yo yote wa Umoja wa Mataifa ambaye hana naibu wa daima katika halmashauri ataitwa na halmashauri aweko pamoja nao itakapokuwa katika kutekeleza vyema wajibu wa halmashauri kunahitajia awemo mwanachama huyo katika kazi zake.

3. Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri ya mambo ya vita kuona chini ya uangalizi wa Baraza la Usalama na kuziongoza kwa njia za kivita nguvu zo zote za silaha zilizo chini ya amri ya Baraza la Usalama. Mambo ya kuziamuru nguvu hizo yatapangwa baadaye.

4. Kwa amri ya Baraza la Usalama na baada ya kushauriana na mawakala wa nchi zinazohusika, halmashauri ya mambo ya vita inaweza kuchagua halmashauri ndogo ndogo katika hizo nchi.

Sehemu ya 48

1. Hatua za kutekeleza hukumu za Baraza la Usalama ya kuhifadhi salama na amani baina ya mataifa itachukuliwa na wanachama wote wa Umoja wa Mataifa au na baadhi yao, kama litavyokata shauri Baraza la Usalama.

2. Hukumu hizo zitatekelezwa na wanachama wa Umoja wa Mataifa moja kwa moja na kwa kuchukua hatua katika wakala za mataifa zinazofaa ambazo wao ni wanachama.

Sehemu ya 49

Wanachama wa Umoja wa Mataifa watachanganyika ili kusaidiana katika kuyatekeleza mambo yaliyoamuliwa na Baraza la Usalama.

Sehemu ya 50

Ikiwa Baraza la Usalama limechukua hatua za kuzuia au za kutumia nguvu juu ya nchi yo yote, nchi yo yote nyingineyo ikiwa ni Mwanachama au Si mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambayo itajiona imekabiliwa na mashaka maalum ya uchumi kutokana na kuchukuliwa hatua hizo itakuwa na haki ya kulishauri Baraza la usalama juu ya njia ya kuyaondoa mashaka hayo.

Sehemu ya 51

Hapana lo lote katika Mkataba huu litalopunguza haki ya asili ya nchi ikiwa ni moja au nyingi ya kujitetea ikiwa mashambulio ya nguvu za silaha yatatokea juu ya mwanachama wa Umoja wa Mataifa mpaka Baraza la Usalama litapochukua hatua za lazima za kuhifadhi salama na amani baina ya mataifa. Baraza la Usalama litaarifiwa mara tu juu ya hatua walizochukua wanachama katika kuitumia haki hii ya kujitetea na hatua hizo hazitogeuza mamlaka na madaraka ya Baraza la Usalama kwa mujibu wa Mkataba huu kuchukua hatua wakati wo wote ule kama

itavyolazimika ili kuhifadhi au kurudisha salama na amani ya mataifa.

SURA YA VIII

MIPANGO BAINA YA MAJIMBO

Sehemu ya 52

1. Hapana lo lote katika katiba hii linalozuia kuwepo mipango au wakala baina ya majimbo ya kuzingatia mambo yanayohusu kuhifadhi salama na amani kama itavyofaa katika majimbo hayo kwa shuruti kuwa mipango hiyo au wakala hizo na shughuli zake ziwe sawa na madhumuni na misingi ya Umoja wa Mataifa.
2. Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaoingia katika mipango hiyo au watakao anzisha wakala hizo watafanya kila bidii, ili kufikilia mapatano ya salama ya ugomvi katika sehemu yao ya majimbo kwa kuitumia hiyo mipango au wakala kabla ya kuupeleka ugomvi huo mbele ya Baraza la Usalama.

3. Baraza la Usalama litatilia nguvu kuwepo mapatano ya salama ya ugomvi wa majimbo kwa kuitumia hiyo mipango au wakala ama kwa kuanzwa mapatano hayo na nchi zinazohusika au kwa maelekezo yatakayotolewa na Baraza la Usalama.

4. Sehemu hii haitopunguza kwa namna yo yo yote kutumika kwa sehemu ya 34 na 35.

Sehemu ya 53

1. Baraza la Usalama litautumia mpango huo wa majimbo au wakala kwa kulazimisha mambo chini ya amri yake litakapoona kuwa inafaa. Lakini hatua yoyote ya kutumia nguvu haiwezi kuchukuliwa chini ya mipango ya majimbo au wakala wa majimbo bila ya ruhusa ya Baraza la Usalama, isipokuwa kama ni kuchukua hatua juu ya nchi adui, kama ilivyoelezwa katika fasili ya 2 ya Sehemu hii, hatua inayoruhusiwa na Sehemu ya 107 au ni katika mipango ya majimbo iliyokusudiwa kuzuia urudishaji upya wa siasa ya uchokozi kwa upande wa nchi yoyote kama hiyo. Mipango ya majimbo na wakala itaendelea kuchukua hatua ya namna hiyo mpaka wakati chama kitakapoweza kuchukua madaraka ya kuzuia uchokozi zaidi wa nchi hiyo kwa kutakiwa na serikali ihusikanayo.

2. Tamko la 'dola adui' lililotumiwa katika fungu la 1 la sehemu hii litahusika na nchi yo yote ambayo katika Vita vya Dunia vya Pili ilikuwa ni adui wa nchi yo yote iliyotia sahihi Mkataba huu.

Sehemu ya 54

Baraza la Usalama litakuwa kila wakati linaarifiwa mambo yanayofanywa au yanayoazimiwa kufanywa kwa mujibu wa mipango au wakala baina ya majimbo kwa kuhifadhi salama na amani baina ya mataifa.

SURA YA IX

USHIRIKIANO WA MATAIFA WA UCHUMI NA MAMBO YA STAREHE

Sehemu ya 55

Kwa kusudi la kutengeneza hali za utulivu na ustawi ambazo ni lazima kwa uhusiano wa salama na urafiki baina ya mataifa hali ambazo zimetegemea msingi wa kuheshimu haki ya usawa na hiari za watu, Umoja wa Mataifa utaendeleza:—

a. Hali za juu za maisha, kuweko kazi kwa wote na hali za uchumi na kukuza mambo ya starehe na maendeleo;

b. Kuondosha matatizo ya mataifa yanayohusu mambo ya uchumi, starehe, afya na matatizo kama hayo; na kushirikiana katika mambo ya utamaduni na elimu ya mataifa; na

c. Kuheshimu na kuchunga kwa ulimwengu juu ya haki za Kibinadamu na misingi ya uhuru kwa wote bila ya ubaguzi wa kabila, mwanamume au mwana mke,lugha au dini.

Sehemu ya 56

Wanachama wote wanajichukulia ahadi ya kuchukua hatua ama kwa umoja au mbali mbali ya kushirikiana na chama ili kufikilia madhumuni yaliyotajwa katika sehemu ya 55

Sehemu ya 57

1. Wakala mbali mbali mahsusi zilizowekwa kwa masikilizano baina ya serikali na serikali na ambazo zina wajibu mkubwa unaohusu mataifa, kama ilivyoelezwa katika hati zao, katika mambo ya uchumi, starehe, utamaduni elimu, afya na mambo kama hayo, zitafanywa zihusiane na Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa masharti ya sehemu ya 63.

2. Wakala hizo ambazo zimefanywa kuhusiana na Umoja wa Mataifa toka hapa zitajulikana kuwa ni wakala mahsusi.

Sehemu ya 58

Chama kitatoa mapendekezo yake ya kuweka sawa sawa siasa na shughuli za hizo wakala mahsusi.

Sehemu ya 59

Kitakapoona inafaa chama kitaanzisha masikilizano baina ya nchi zinazohusika juu ya kuunda wakala mahsusi mpya zinazohitajika kwa kukamilisha madhumuni yaliyotajwa katika Sehemu ya 55.

Sehemu ya 60

Madaraka ya kuzitekeleza kazi za chama zilizotajwa katika Sura hii yatakabidhiwa Baraza Kuu na kwa mamlaka ya Baraza Kuu.

yatakabidhiwa Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe ambalo kwa madhumuni haya litakuwa na uwezo ulitajwa katika Sura ya X.

SURA YA X

HALMASHAURI YA UCHUMI NA USTAWI WA JAMII

Muundo wake

Sehemu ya 61

1. Halmashauri ya Uchumi na Ustawi wa Jamii itakuwa na wajumbe hamsini na nne wa wanachama wa Umoja wa Mataifa, watakaochaguliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

2. Kwa kufuata kanuni za kifungu cha 3, wajumbe 18 watachaguliwa kila mwaka katika Halmashauri ya Uchumi na Ustawi wa Jamii, kushika madaraka ya miaka mitatu. Wajumbe watakaomaliza muda wao wanaweza kuchaguliwa tena, ikiwa wanahitajiwa.

3. Katika uchaguzi wa kwanza, baada ya kuzidishwa idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Uchumi na Ustawi wa Jamii kutoka 27 na kuwa 57 na zaidi ya wajumbe waliochaguliwa badala ya wajumbe 9 waliomaliza muda wao mwisho wa mwaka, wajumbe wengine 27 watachaguliwa. Katika Wajumbe

hao 27, muda wa madaraka ya wajumbe tisa watakaochaguliwa hivyo, utamalizika baada ya mwaka mmoja tu, wajumbe wengine tisa baada ya miaka miwili, kwa kufuata mipango iliyotayarishwa na Baraza Kuu.

4. Kila nchi iliyo mwanachama wa Halmashauri ya Uchumi na Ustawi wa Jamii, itakuwa na mjumbe mmoja tu.

Kazi na Uwezo:

Sehemu ya 62

1. Baraza la mambo ya Uchumi na starehe linaweza kutengeneza au kuanzisha masomo na taarifa zinazohusu uchumi wa mataifa starehe, utamaduni, elimu, afya na mengineo kama hayo na linaweza kutoa mapendekezo yake juu ya mambo yo yote kama hayo kwa Baraza Kuu, kwa wanachama wa Umoja wa Mataifa na kwa wakala mahsusi zilizohusika.

2. Linaweza kutoa mapendekezo yake kwa madhumuni ya kuleta heshima na kuchunga haki za binadamu na misingi ya uhuru kwa wote.

3. Linaweza kutengeneza mapatano juu ya mambo yaliyo chini yake na kuyapeleka mbele ya Baraza Kuu kufikiriwa.

4. Linaweza kuita mikutano ya mataifa juu

ya mambo yalio chini yake kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 63

1. Baraza la mambo ya uchumi na starehe linaweza kuingia katika mikataba na wakala yo yote katika zile zilizotajwa katika Sehemu ya 57, kwa kufafanua shuruti ambazo hiyo wakala iliyohusika itafanya ihusiane na Umoja wa Mataifa, Mikataba hiyo itabidi ikubaliwe na Baraza Kuu.

2. Linaweza kusawazisha shughuli za wakala mahsusi kwa kushauriana na kupeleka mapendekezo yake kwa wakala hizo na kwa kupeleka mapendekezo yake kwa Baraza Kuu na kwa wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 64

1. Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe linaweza kuchukua hatua zinazofaa ili lipate taarifa kila mara kutoka kwa wakala mahsusi. Linaweza kufanya mipango na wanachama wa Umoja wa Mataifa na wakala mahsusi ili lipate taarifa juu ya hatua zilizochukuliwa katika kutimiza mapendekezo yake na mapendekezo ya Baraza Kuu juu ya mambo yalio chini yake.

2. Linaweza kupeleka maoni yake juu ya taarifa hizi kwa Baraza Kuu.

Sehemu ya 65

Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe linaweza kulipelekea habari Baraza la Usalama na litasaidia Baraza la Usalama litakapoomba msaada.

Sehemu ya 66

1. Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe litafanya kazi ambazo zipo chini yake katika kuyatekeleza mapendekezo ya Baraza Kuu.

2. Linaweza, kwa idhini ya Baraza Kuu, kufanya kazi kwa kuombwa na wanachama wa Umoja wa Mataifa na kwa kuombwa na wakala mahsusi.

3. Litafanya kazi nyinginezo kama zitakazotajwa mahala penginepo katika Mkataba huu au kama litakazopewa na Baraza Kuu.

Kupiga Kura:

Sehemu ya 67

1. Kila mwanachama wa Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe atakuwa na kura moja.

2. Uamuzi wa Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe utafanywa kwa kutegemea kupatikana kura nyingi kutokana na wanachama watakaokuwepo na kupiga kura zao.

Utaratibu:

Sehemu ya 68

Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe litaweka halmashauri katika mambo ya uchumi na starehe na ya kuendeleza haki za binadamu na halmashauri nyinginezo zitakazohitajiwa kwa kufanya kazi zake.

Sehemu ya 69

Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe litamualika mwanachama yo yote wa Umoja wa Mataifa awemo, bila ya kuwa na kura, katika mashauriano yake juu ya jambo lo lote ambalo linamhusu mwanachama huyo.

Sehemu ya 70

Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe linaweza kufanya mipango ili wajumbe wa wakala mahsusi wawemo, bila ya kuwa na kura, katika mashauriano yake na ya halmashauri iliozíweka, na mpango kwa wajumbe wake ili wawemo katika mashauriano ya wakala mahsusi.

Sehemu ya 71

Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe linaweza kufanya mipango inayofaa ya kushauriana na vyama visivyokuwa vya serikali ambavyo vimehusika na mambo yaliopo chini

yake. Mipango kama hiyo inaweza kufanywa na vyama vya mataifa na itapofaa, na vyama vinavyohusu taifa moja baada ya kushauriana na mwanachama wa Umoja wa Mataifa anayehusika.

Sehemu ya 72

1. Baraza la mambo ya Uchumi la Starehe, litaweka kanuni na mipango yake pamoja na namna ya kumchagua Rais wake.

2. Baraza la mambo ya Uchumi na Starehe litakutana kama itavyohitajikana kwa mujibu wa kanuni zake ambazo itakuwemo sharti ya kuitwa mikutano kwa kuomba idadi kubwa ya wanachama wake.

SURA YA XI

TANGAZO LINALOHUSU NCHI ZILIZOJITAWALA

Sehemu ya 73

Wanachama wa Umoja wa Mataifa ambao wanao au wamechukua madaraka ya kuendesha serikali ya nchi ambazo watu wake bado kufikilia daraja kamili ya kujitawala wanatambua msingi usemao kwamba masilahi ya wakazi wa nchi hizi ni jambo muhimu sana kupita yote, na wanakubali kuwa ni dhamana takatifu kwa wajibu wa kuendeleza kama

wawezavyo, bila ya kuuvuka mpango wa salama na amani wa mataifa ulioanzishwa na Mkataba huu, usitawi wa wakazi wa nchi hizi, na kwa kuyafikilia haya wanakubali:—

a. kuhakikisha kuwa wametendewa haki na kuhifadhiwa na matusi na kuheshimu utamaduni wa watu hao, maendeleo yao ya siasa, uchumi, starehe na elimu.

b. Kuendeleza hali ya kujitawala, kuzingatia kama inavyositahiki matakwa ya watu juu ya mambo ya siasa, na kuwasaidia katika maendeleo yao ya vyama huru vya siasa, kwa mujibu wa hali ya kila nchi, watu wake na daraja zao mbali mbali za maendeleo;

c. Kuendeleza mbele salama na amani ya mataifa;

d. Kuendeleza mipango madhubuti ya koendeleza mbele, kutiliwa nguvu mambo ya uvumbuzi, na kushirikiana baina yao na inapokuwa inafaa na vyama mahsusi vya mataifa kwa madhumuni ya kufaulu kisiasa juu ya starehe, uchumi na maarifa yaliyotajwa katika sehemu hii, na

e. kupeleka kila mara kwa Katibu Mkuu, kwa madhumuni ya kumpasha habari, kwa kufuata kiwango kinachotakiwa kwa usalama na kufuata Katiba, hesabu na habari nyinginezo za kifundi kuhusu mambo ya uchumi, starehe na hali ya elimu katika nchi

ambazo zimo chini yao zisizokuwa nchi zile ambazo Sura ya XII na XIII zinahusika.

Sehemu y 74

Wanachama wa Umoja wa Mataifa vile vile wanakubali kuwa siasa yao juu ya nchi ambazo zinahusika na Sura hii, siasa yao ilivyo juu ya nchi zao lazima ifuate msingi wa kawaida wa ujirani mwema na kuzingatiwa vilivyo masilahi na usitawi wa schemu nyingine za dunia zilizobaki katika mambo ya starehe, uchumi na biashara.

SURA YA XII

MPANGO WA UDHAMINI WA MATAIFA

Sehemu ya 75

Umoja wa Mataifa utaweka chini ya mamlaka yake mpango wa kudhamini mataifa kwa kuendesha kazi na kuangalia nchi ambazo zinaweza kuwekwa chini ya mpango huo kwa kufuata mapatano ya kila mojawapo. Nchi hizi ndizo zitakazojulikana kama za udhamini.

Sehemu ya 76

Nia ya Udhamini wa Mataifa kwa kufuata madhumuni ya Umoja wa Mataifa kama

yalivyoelezwa katika sehemu ya kwanza ya Mkataba huu ni:

a. Kuendeleza amani na salama ya mataifa.

b. Kuendeleza siasa, uchumi, hali na elimu ya wenyeji wa nchi zilizo chini ya udhamini na maendeleo yao kuelekea kupata madaraka katika kuendesha serikali au uhuru kadiri itakavyokuwa kwa kufuata hali ya nchi inayohusika na watu wake na matakwa ya watu wenyewe, na kama itakavyoruhusiwa na masharti ya kila mapatano ya udhamini.

c. Kutia nguvu juu ya heshima za haki za wanadamu na kanuni za uhuru wa kila mtu bila kujali utaifa, mwanamke au mwanamume, lugha au dini na kutia nguvu kutambulikana kwa kutegemeana kwa walimwengu; na

d. Kuhakikisha usawa kwa matendo katika mambo ya furaha, uchumi na mambo yanayohusika na biashara kwa wanachama wote wa Umoja wa Mataifa na raia wao, na pia kutendewa usawa kwao hao katika kutimiza uadhilifu, bila ya kuharibu kupatikana kwa madhumuni yanayotajwa na kwa kufuata masharti ya sehemu ya 80.

Sehemu ya 77

1. Mpango wa Udhamini wa Mataifa utahusu nchi ambazo zinaweza kuwa chini

ya jamii zifuatazo kwa kufuata mapatano ya udhamini.

a. Nchi ambazo hivi sasa zimo chini ya Ushirika wa Mataifa.

b. Nchi ambazo zinaweza kuondolewa toka madola ya adui kutokana na matokeo ya Vita Kuu ya Pili; na

c. Nchi ambazo zimewekwa kwa hiyari chini ya mpango huu na nchi zinazohusika na kuzitawala.

2. Litakuwa ni jambo la mpatano ya hatimaye kwamba ni nchi gani kutokana na jamii hizo ambazo zitawekwa chini ya mpango wa udhamini na kwa kufuata kanuni zipi.

Sehemu ya 78

Mpango wa Udhamini hautahusika na nchi ambazo zimejiunga na Umoja wa Mataifa, ambazo uhusiano wao utategemea heshima ya usawa wa taifa.

Sehemu ya 79

Masharti ya udhamini kwa kila nchi itakayowekwa chini ya mpango wa udhamini, pamoja na mageuzo au mabadiliko yatabidi yakubaliwe na Mataifa yanayohusika hasa, na kuchanganya mamlaka ya kutawala nchi zilizo chini ya mpango wa Ushirika ambazo mtawala

wake ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na ni lazima zipate idhini kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 83 na 85.

Sehemu ya 80

1. Isipokuwa kama itakavyokubaliwa na kila mojawapo ya mapatano ya udhamini kama yalivyo katika sehemu ya 77, 79 na 81, yakiweka kila nchi chini ya mpango wa udhamini, na mpaka hapo mapatano hayo yatakapomalizwa, hakuna chochote katika Sura hii kinachoweza kufasiriwa au chenyewe kubadili kwa namna yoyote haki za nchi yoyote au watu au masharti ya hati zilizopo zinazohusu mataifa mbali mbali ambazo wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaweza kuhusika.

2. Fasili ya kwanza ya sehemu hii haitaeleweka kama ndio chanzo cha kuchelewesha au kuahirisha maafikiano na kumaliza mapatano ya kuweka nchi zilizo chini ya Ushirika na nyinginezo chini ya Mpango wa Udhamini kama ilivyowekwa katika sehemu ya 77.

Sehemu ya 81

Mapatano ya Udhamini mara zote yatachanganya na masharti ambayo kwayo nchi ya udhamini itakavyotawaliwa na pia kuteua nchi ambayo itashika utawala wa nchi ya udhamini. Nchi hiyo basi, ndiyo itakayojulikana kama nchi inayotawala, nayo yaweza

kuwa moja, au zaidi ya moja, au pengine Umoja wa Mataifa wenyewe.

Sehemu ya 82

Inaweza kuchaguliwa sehemu inayofaa au zinazofaa kwa majeshi ya vita katika mapatano yoyote ya udhamini, ambayo inaweza kuwa ni sehemu au nchi yote ya udhamini ambayo kwayo mapatano hayo yanahusu, bila kuharibu mapatano maalum au mapatano yoyote yaliyofanywa chini ya Sehemu ya 43.

Sehemu ya 83

1. Shughuli zote za Umoja wa Mataifa zinazohusu sehemu zinazofaa kwa majeshi ya vita, pamoja na idhini ya masharti ya mapatano ya udhamini na mabadiliko au masahihisho yake, yatashughulikiwa na Baraza la Usalama.

2. Madhumuni yaliyomo katika Sehemu ya 76 yatawahusu watu wa kila sehemu inayofaa kwa majeshi ya vita.

3. Baraza la Usalama, kwa kufuata masharti ya mapatano ya udhamini na bila kuharibu, nadhari ya Usalama, litafaidika na msaada wa Baraza la Udhamini katika kutimiza shughuli za Umoja wa Mataifa chini ya mpango wa udhamini unaohusu mambo ya siasa, uchumi, hali za watu na mambo ya elimu katika sehemu zinazofaa kuweka majeshi ya vita.

Sehemu ya 84

Itakuwa ni wajibu wa nchi inayotawala kuhakikisha kwamba nchi ya Udhamini itapata nafasi ya kushiriki katika shughuli za kudumisha amani na usalama kati ya mataifa. Ikiwa na shabaha hii nchi inayotawala inaweza kutumia majeshi yanayojitolea, njia na misaada inayotolewa na nchi ya udhamini katika kutimiza wajibu wake kwa Baraza la Usalama uliochukuliwa na nchi inayotawala, hali kadhalika kwa ulinzi na utunzaji wa sheria na amani katika nchi ya udhamini.

Sehemu ya 85

1. Kazi za Umoja wa Mataifa kuhusiana na mapatano ya udhamini kwa sehemu zote ambazo hazikuteuliwa kuwa ni sehemu zinazofaa kwa majeshi ya vita, pamoja na idhini ya masharti ya mapatano ya udhamini na mabadiliko yake au masahihisho, zitafanywa na Baraza Kuu.

2. Baraza la Udhamini, likifanya kazi kwa kufuata amri za Baraza Kuu, litalisaidia Baraza Kuu katika kuzitimiza shughuli hizi.

SURA YA XIII

BARAZA LA UDHAMINI

UMBO.

Sehemu ya 86

1. Baraza la Udhamini litakuwa na wanachama wa Umoja wa Mataifa wafuatao:

a. Wanachama wale wanaotawala nchi za udhamini.

b. Wale wanachama waliotajwa kwa majina katika sehemu ya 23 na ambao hawatawali nchi za udhamini; na

c. Wanachama wengine watakaochaguliwa na Baraza Kuu kuwamo kwa muda wa miaka mitatu kwa kadiri itakavyokuwa lazima kuhakikisha kwamba jumla ya wanachama wa Baraza la Udhamini imegawanywa sawa kati ya wanachama wa Umoja wa Mataifa ambao wanatawala nchi za udhamini na wale ambao si watawala.

2. Kila nchi iliyo mwanachama wa Baraza la Udhamini itachagua mjumbe wake mwenye ujuzi maalum aiwakilishe katika Baraza hilo.

Sehemu ya 87

Baraza Kuu na Baraza la Udhamini, chini ya uongozi wa Baraza Kuu, wakati wa kutimiza shughuli zake laweza:

a. Kufikiria taarifa zitakazotolewa na nchi inayotawala;

b. Kupokea malalamiko na kuyachungua kwa kushauriana na nchi inayotawala;

c. Kutengeneza mpango wa kuzitembelea nchi za udhamini katika nyakati zitakazokubaliwa na nchi inayotawala, na

d. Kufanya haya na mengineyo kwa mujibu wa mapatano ya udhamini.

Sehemu ya 88

Baraza la Udhamini litadadisi juu ya maendeleo ya siasa, uchumi, hali za watu na elimu ya wenyeji au watu wa kila nchi ya udhamini, na kila nchi inayotawala nchi ya udhamini kwa nguvu za Baraza Kuu italazimika kutoa taarifa ya kila mwaka mbele ya Baraza Kuu kwa kufuata udadisi ulivyo.

Kupiga Kura:

Sehemu y 89

1. Kila nchi iliyo mwanachama wa Baraza la Udhamini itakuwa na kura moja.

2. Maamuzi ya Baraza la Udhamini yatakuwa kwa kufuata kura nyingi zilizopigwa na wanachama waliopo.

Utaratibu

Sehemu ya 90

1. Baraza la Udhamini litaweka masharti yake yenyewe juu ya utaratibu wake, pamoja na njia ya kuteua Rais wake.

2. Baraza la Udhamini litakutana kama inavyotakikana na masharti yake, pamoja na madaraka ya kuitisha mikutano itakapotakiwa na wingi wa wanachama wake.

Sehemu ya 91

Baraza la Udhamini, kila itakapofaa, litakuwa tayari kupokea misaada toka kwa Baraza la Uchumi na Starehe na kutoka kwa makundi maalumu kuhusu mambo ambayo kwayo yanayashughulikia.

SURA YA XIV

MAHAKAMA YA MATAIFA YA ULIMWENGU

Sehemu ya 92

Mahakama ya Mataifa ya Ulimwengu ndiyo itakayokuwa sehemu maalum ya uadilifu ya Umoja wa Mataifa. Itafanya kazi zake kwa kufuata sheria iliyoongezwa, ambayo msingi wake ni sheria ya Mahakama ya Kudumu ya Mataifa ya Ulimwengu na ambayo ni sehemu kamilifu ya Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 93

1. Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa moja kwa moja wamo chini ya Sheria ya Mahakama ya Mataifa ya Ulimwengu.

2. Nchi ambayo si mwanachama wa Umoja wa Mataifa inaweza kuwamo chini ya Mahakama ya Mataifa ya Ulimwengu kwa masharti ambayo yatatolewa na Baraza Kuu likishauriwa na Baraza la Usalama juu ya kila jambo.

Sehemu ya 94

1. Kila nchi iliyo mwanachama wa Umoja wa Mataifa ina wajibu wa kufuata uamuzi uliopitishwa na Mahakama ya Mataifa ya Ulimwengu kuhusu kesi yoyote ambayo nchi hiyo ni mdaawa.

2. Mdaawa yoyote wa kesi fulani akiacha kutimiza yale ambayo yanambidi kufanya kwa kufuata hukumu iliyotolewa na Mahakama, mdaawa mwingine aweza kukimbilia kwa Baraza la Usalama ambalo iwapo litaona ni lazima laweza kutoa mapendekezo au kukata shauri juu ya hatua inayopaswa kufuatwa ili kutimiza hukumu iliyotolewa.

Sehemu ya 95

Hakipo chochote katika Mkataba huu ambacho kitaweza kuwazuia wanachama wa Umoja wa Mataifa wasiweze kukabidhi uamuzi wa matatizo yao mikononi mwa mabaraza mengine kwa uwezo wa maafikiano ambayo yamekwisha kuwepo au yatakayofikiwa hapo baadaye.

Sehemu ya 96

1. Baraza Kuu au Baraza la Usalama linaweza kuiomba Mahakama ya Mataifa ya Ulimwengu kutoa maoni ya kushauri juu ya jambo lolote la kisheria.

2. Matawi mengine ya Umoja wa Mataifa na makundi mengine maalum, ambayo wakati wowote yaweza kuruhusiwa na Baraza Kuu, pia yaweza kuomba maoni ya kushauri ya Mahakama liyo juu ya mambo ya sheria ambayo yanatokana na shughuli zao.

SURA YA XV

AFISI KUU

Sehemu ya 97

Afisi Kuu ya Umoja wa Mataifa itakuwa na Katibu Mkuu na watumishi wengine ambao Umoja wa Mataifa utahitaji. Katibu Mkuu atateuliwa na Baraza Kuu kwa kufuata mapendekezo ya Baraza la Usalama. Yeye ndiye atakayekuwa afisa mkuu asimamiaye kazi zote za Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 98

Katibu Mkuu atafanya kazi katika hali hiyo kwenye mikutano yote ya Baraza Kuu, Baraza la Usalama, Baraza la Uchumi na Starehe, na pia katika Baraza la Udhamini, na atafanya kazi nyingine zote atakazokabidhiwa na mabaraza hayo. Katibu Mkuu atatayarisha taarifa ya mwaka itakayotolewa mbele ya Baraza Kuu kuhusu kazi zote za Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 99

Katibu Mkuu anaweza kulijulisha Baraza la Usalama jambo lolote ambalo kwa maoni yake linaweza kuleta hali ya wasiwasi katika kulinda amani na usalama wa Mataifa ya Ulimwengu.

Sehemu ya 100

1. Katika kutenda kazi zao, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wengine wa Umoja wa Mataifa hawana ruhusa kuomba au kupokea amri toka kwa serikali yoyote au toka kwenye mamlaka nyingine yoyote ambayo haimo katika Umoja wa Mataifa. Wao watajiepusha na shughuli yoyote ambayo yaweza kushutumu hali yao wakiwa watumishi wa Mataifa ya ulimwengu chini ya Umoja wa Mataifa.

2. Kila mwanachama wa Umoja wa Mataifa ni wajibu wake kuheshimu Mkataba wa pekee wa mataifa ya ulimwengu juu ya madaraka ya Katibu Mkuu na watumishi na haruhusiwi kuwashawishi juu ya utumiaji wa madaraka yao.

Sehemu ya 101

1. Watumishi watateuliwa na Katibu Mkuu kwa kufuata mpango uliowekwa na Baraza Kuu.

2. Watumishi wanaofaa watawekwa daima kwenye baraza la Uchumi na Starehe, Baraza la Udhamini na kama itakavyohitajiwa katika sehemu nyingine za Umoja wa Mataifa. Watumishi hawa watakuwa ni baadhi ya watumishi wa Afisi Kuu.

3. Jambo kubwa litakalofikiriwa katika kuajiri watumishi na katika kuweka hali za kazi litakuwa ni umuhimu wa kupata utendaji

bora wa kazi, ustadi na uaminifu. Uwezekano wa kuajiri watumishi kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu utakuwa maanani.

SURA YA XVI

MASHARTI MENGINEO

Sehemu ya 102

1. Kila Mkataba wa kila mapatano ya nchi za Ulimwengu ambayo mwanachama yoyote wa Umoja wa Mataifa atahusika baada ya Mkataba huu kuanza kutumika, utabidi uingizwe katika daftari la Afisi Kuu na kutangazwa nayo kwa haraka iwezekanavyo.

2. Hakuna upande wowote unaohusika na Mkataba huo au mapatano ya nchi za Ulimwengu ambayo hayakuingizwa daftarini kwa kufuata fasili ya kwanza ya sehemu hii utakaoruhusiwa kutumika katika tawi lolote la Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 103

Inapotokea kuhitilafiana juu ya wajibu wa wanachama wa Umoja wa Mataifa chini ya Mkataba uliopo na juu ya wajibu wao kuhusu mapatano mengine yoyote ya nchi za ulimwengu, wajibu wao chini ya Mkataba uliopo ndio utakaofuatwa.

Sehemu ya 104

Umoja wa Mataifa utakuwa huru kutumia uwezo wake wa kisheria kama itakavyopasa, kutenda kazi zake na kutimiza makusudi yake katika nchi yoyote iliyo mwanachama wa Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 105

1. Umoja wa Mataifa katika kila nchi iliyo mwanachama wake, utapata heshima na uhuru kama unaopasika kwa kutimiza makusudi yake.
2. Wajumbe wa nchi zilizo wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Watumishi wa Umoja huo pia watapewa heshima kama hizo na uhuru kama huo ili waweze kufanya kazi zao zinazohusika na Umoja wa Mataifa bila ya kuingiliwa.
3. Baraza Kuu linaweza kutoa mapendekezo ambayo yataeleza jinsi fasili ya kwanza na ya pili ya sehemu hii zinavyoweza kutumika au laweza kutoa mashauri juu ya maafikiano kwa wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu jambo hili.

SURA YA XVII

MIPANGO YA MUDA YA USALAMA

Sehemu ya 106

Kabla ya kuanza kutumika kwa mapatano maalum yaliyotajwa katika Sehemu ya 43

kwa maoni ya Baraza la Usalama kuliwezesha kuanza kutimiza madaraka yake kwa kufuata Sehemu ya 42. wanaohusika na Taarifa ya Mataifa-Manne iliyotiwa sahihi huko Moscow, mnamo tarehe 30 Oktoba, 1943, na Ufaransa, kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Taarifa hiyo, watashauriana wenyewe na wanachama wengine wa Umoja wa Mataifa, kwa jinsi hali itakavyokuwa ili kuchukua hatua ya pamoja kwa niaba ya Umoja wa Mataifa kama itakavyobidi kudumisha amani na usalama wa Mataifa.

Sehemu ya 107

Kwa kadri Mkataba ulivyo hivi sasa, hakuna chochote kitakacho batilisha ua kuzuia kitendo kitakachofanywa au kuruhusiwa kwa kutokana na vita kuu ya pili na Serikali zenye Madaraka ya kitendo hicho kuhusu nchi yoyote ambayo wakati wa vita hiyo ilikuwa ni adui ya nchi yoyote iliyotia sahihi katika mkataba wa sasa.

SURA YA XVIII

MABADILISHO

Sehemu ya 108

Mabadilisho juu ya Mkataba wa sasa yatahusu wanachama wote wa Umoja wa Mataifa mara tu yanapokubaliwa kwa kura zenye idadi ya theluthi mbili za wanachama

wa Baraza Kuu na yakiidhiniwa kwa kufuata kanuni zao kwa theluthi mbili za wanachama wa Umoja wa Mataifa, pamoja na wanachama wote wa kudumu wa Baraza la Usalama.

Sehemu ya 109

1. Mkutano wa wanachama wa Umoja wa Mataifa wa kuchungua Mkataba waweza kufanywa katika tarehe na mahala patakapowekwa kwa uamuzi wa kura zenye idadi ya theluthi mbili za wanachama wa Baraza Kuu na kwa kuwa kura za wanachama wowote tisa wa Baraza la Usalama. Kila mwanachama wa Umoja wa Mataifa atakuwa na kura moja tu katika mkutano huu.

2. Mageuzo yoyote ya Mkataba uliyopo yatakayopendekezwa na theluthi mbili ya kura za mkutano yataanza kutumika hapo yatakapoidhinishwa kwa kufuata kanuni zao za theluthi mbili za kura za wanachama wa Umoja wa Mataifa pamoja na wanachama wote wa kudumu wa Baraza la Usalama.

3. Kama mkutano kama huo haukufanyika kabla ya kikao cha kumi cha mwaka cha Baraza Kuu baada ya Mkataba huu kuanza kutumika, shauri la kuita mkutano kama huo litawekwa katika orodha ya mambo ya mkutano ya kikao hicho cha Baraza Kuu, na mkutano unaweza kufanywa kama ikikubaliwa na kura nyingi zaidi za wanachama wa Baraza Kuu na kwa kura za wanachama saba wowote wa Baraza la Usalama.

SURA YA XIX

MAIDHINISHO NA SAHIHI

Sehemu ya 110

1. Mkataba uliopo utaidhinishwa na wote waliotia sahihi kwa kufuata kanuni zake.

2. Maidhinisho yatakabidhiwa serikali ya Amerika, ambayo itaijulisha kila nchi iliyotia sahihi katika kila uwekaji na pia itamjulisha Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atakapokuwa ameteuliwa.

3. Mkataba huu utaanza kutumika baada ya uwekaji wa maidhinisho ya Jamhuri ya Uchina, Ufaransa, Urusi, Mwungano wa Uingereza na Ireland ya Kaskazini na Amerika na ya nchi nyingi zinazotia sahihi. Mpango wa uwekaji wa maidhinisho utaandikwa na Serikali ya Amerika ambayo itapeleka nakala zake kwa nchi zote zilizotia sahihi.

4. Nchi zilizotia sahihi Mkataba uliopo ambazo zinainidhisha baada ya kuanza kutumika watakuwa ndio wanachama wa Asili wa Umoja wa Mataifa tangu tarehe ya uwekaji wa maidhinisho yao.

Sehemu ya 111

Maandishi ya Mkataba uliopo kwa Kichina, Kifaransa, Kirusi, Kiingereza, au

Kihispania ambapo yote ni rasmi, yatabaki katika kabidhi ya mahala patunzwapo hati na tarehe katika milki ya Serikali ya Amerika.

Serikali ya Amerika itazipeleka nakala zote zilizothibitishwa kwa serikali za nchi nyingine zote zilizotia sahihi.

KWA IMANI AMBAYO KWAYO wajumbe wa serikali za Umoja wa Mataifa wametia sahihi zao katika Mkataba uliopo.

ILIFANYIKA huko katika jiji la San Francisco, tarehe ishirini na sita ya mwezi Juni, mwaka wa Elfu moja mia tisa na arobaini na tano.

SHERIA YA MAHAKAMA YA MATAIFA

Sehemu ya 1

MAHAKAMA YA MATAIFA iliyokubaliwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa ili iwe ni njia muhimu, ya kuhukumu, ya Umoja wa Mataifa itawekwa na itafanya kazi kwa kufuata masharti ya Sheria iliyopo.

SURA YA I

TARATIBU YA MAHAKAMA HIYO

Sehemu ya 2

Mahakama hiyo itakuwa na jamii ya makadhi wasiopendelea upande wowote watakaochaguliwa kutokana na watu wenye tabia bora za kiutu bila kuangalia ni wa taifa gani, na ambao wanazo sifa zinazohitajiwa katika nchi zao kuweza kuchaguliwa katika vyeo vya juu kabisa vya kimahakama au ni wanasheria wa uhodari wanaotambulikana na sheria za mataifa.

Sehemu ya 3

1. Mahakama hiyo itakuwa na wanachama kumi na tano na katika hao haitakubaliwa wanachama wawili wawe ni wa taifa moja.

2. Mtu ambaye kwa madhumuni ya uwanachama wa Mahakama hii atakuwa ni mwananchi wa taifa zaidi ya moja atahesabiwa kuwa ni mwananchi wa lile taifa ambalo kwa kawaida anatumia haki zake za uraia na za siasa.

Sehemu ya 4

1. Wanachama wa Mahakama hii watachaguliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama kutoka katika orodha ya watu walioteuliwa na vikundi vya mataifa katika Mahakama ya Uamuzi ya Kudumu, kwa kufuata masharti haya yafuatayo,

2. Kwa upande wa Wajumbe wa Umoja wa Mataifa ambao hawana wajumbe katika hiyo Mahakama ya Uamuzi ya Kudumu wagombea uchaguzi watateuliwa na vikundi vya mataifa vitakavyochaguliwa na serikali zao kwa ajili hii kwa mujibu wa masharti yale yale yaliyowekwa na Sehemu ya 44 ya Mkataba wa Hague wa 1907 wa kupatanisha migogoro ya mataifa kwa kuchagua wajumbe wa Mahakama ya Uamuzi ya Kudumu.

3. Masharti ambayo kwayo nchi, ambayo inahusika na sheria hii iliyopo lakini si mwanachama wa Umoja wa Mataifa, inaweza kujiingiza katika kuchagua wanachama wa Mahakama hiyo, iwapo hakuna mapatano maalum, yanaweza kuwekwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa mapendekezo ya Baraza la Usalama.

Sehemu ya 5

1. Katika muda usiopungua miezi mitatu kabla ya tarehe ya uchaguzi, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atapeleka maombi ya maandishi kwa wanachama wa Mahakama ya Uamuzi wa Kudumu ambao wamo katika Sheria hii iliyopo, na kuwapeleka wanachama wa vikundi vya mataifa vilivyochaguliwa kwa wajibu wa sehemu ya 4 fasiliya 2 kuwataka watadariki, ndani ya muda watakaopewa, uteuzi wa watu watakaoweza na watakaokuwa tayari kukubali kazi ya wanachama wa Mahakama hiyo.

2. Hakuna kikundi kitakachoruhusiwa kuteua zaidi ya watu wanne, wala kuchagua zaidi ya watu wawili ambao ni wataifa lao. Kwa hali yo yote idadi ya wagombea uchaguzi walioteuliwa na kikundi kimoja isizidi maradufu ya idadi ya viti vitakavyojazwa.

Sehemu ya 6

Kabla ya kufanya uteuzi huu kila kikundi cha taifa kinapendekezwa kushauri Mahakama yake kuu kabisa ya sheria, vyuo na shule zake za sheria na vyuo vikuu vyake vya taifa na matawi ya kitaifa ya vyuo vikuu vya ulimwengu ambayo vinashughulikia elimu ya sheria.

Sehemu ya 7

1. Katibu Mkuu atatayarisha orodha ya majina ya watu walioteuliwa kwa kufuata A-BE-CHE-DE. Hawa tu ndio watakaokuwa na haki ya kuchaguliwa isipokuwa kwa kufuata sehemu ya 12 fasili 2.

2. Katibu Mkuu ataipeleka orodha hii kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama.

Sehemu ya 8

Baada ya hapo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama kila moja litachagua wanachama wa Mahakama bila kutegemea uamuzi wa jingine.

Sehemu ya 9

Katika kila uchaguzi, wachaguaji ni lazima wakumbuke kuwa sio kwamba watu wote watakaochaguliwa kila mmoja awe na sifa zinazotakiwa tu bali pia wakumbuke kwamba katika jumla ya watu watakaochaguliwa uwakilishaji wa namna bora za utamaduni na misingi ya njia za sheria za ulimwengu ni lazima uhakikishwe.

Sehemu ya 10

1. Wale wagombea uchaguzi watakaopata wingi uliokamilika wa kura katika Baraza Kuu

la Umoja wa Mataifa na katika Baraza la Usalama watahesabiwa kuwa wamechaguliwa.

2. Kura yo yote katika Baraza la Usalama iwe ni ya uchaguzi wa makadhi au ya kuchagua wajumbe katika mkutano unaofikiriwa katika sehemu ya 12, kura hiyo itakubaliwa bila ya kubagua kati ya wajumbe wa kudumu na wajumbe wasiodumu wa Baraza la Usalama.

3. Itakapotokea kwamba wananchi zaidi ya mmoja wa taifa moja wakapata uwingi mkamilifu wa kura katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na katika Baraza la Usalama ni yule tu mwenye umri kuwapita wote ndiye atakayehesabiwa kuwa amechaguliwa.

Sehemu ya 11

Ikiwa baada ya mkutano wa kwanza wa kufanya uchaguzi pataonekana kuwa kiti kimoja au zaidi vimebaki havijajazwa, basi utafanywa mara ya pili na ikilazimu hata mara ya tatu.

Sehemu ya 12

1. Ikiwa baada ya mkutano wa mara ya tatu kumebakiwa kiti kimoja au zaidi vinavyotaka kujazwa, mkutano wa shirika utakaokuwa na wajumbe sita, watatu watakaochaguliwa na Baraza Kuu na watatu watakaochaguliwa na Baraza la Usalama, utafanywa wakati wowote utakapotakiwa ama na Baraza

Kuu ama Baraza la Usalama kwa madhumuni ya kuchagua kwa kura ya wingi kwa ukamilifu jina moja kwa kila kiti kilichowazi na kupeleka jina au majina hayo kwenye Baraza Kuu na Baraza la Usalama ili mabaraza hayo yakubali.

2. Ikiwa mkutano huu wa shirika umekubaliana kwa umoja kumchagua mtu anayeyatimiza masharti yanayohitajiwa anaweza kutiwa katika orodha ya watu walioteuliwa kama ilivyotajwa katika Sehemu ya 7.

3. Ikiwa mkutano huo wa shirika utatosheka na kuona kwamba hauwezi kufaulu katika kufanya uchaguzi wale wanachama wa Mahakama waliokwisha kuwa wamechaguliwa wataendelea kujaza viti vilivyo wazi, katika muda watakaopewa na Baraza la Usalama, kwa kuchagua kutokana na wale wagombea uchaguzi waliopata kura ama katika Baraza Kuu au katika Baraza la Usalama.

4. Itakapotokea usawa wa kura kati ya makadhi, yule kadhi mwenye umri wa kuwapita wote ndiye atakayekuwa na kura ya kukata shauri.

Sehemu ya 13

1. Wanachama wa Mahakama watachaguliwa na watakaa kwa muda wa miaka tisa na baada ya hapo wanaweza kuchaguliwa tena isipokuwa kwamba katika makadhi walio-

chaguliwa katika uchaguzi wa mara ya kwanza muda wa makadhi watano utakwisha baada ya kumalizika miaka mitatu na muda wa makadhi watano zaidi utamalizika baada ya kwisha miaka sita.

2. Makadhi wale ambao muda wao utamalizika baada ya kwisha miaka hiyo ya mwanzo iliyotajwa hapo juu yaani miaka mitatu na miaka sita, watachaguliwa kwa njia ya kura itakayofanywa na Katibu Mkuu mara baada ya uchaguzi wa mwanzo kumalizika.

3. Wanachama wa Mahakama hiyo wataendelea kufanya kazi zao mpaka mahali pao pamewekwa watu wengine. Ingawaje watawekwa watu wengine badala yao itawalazimu kumaliza kesi zao ambazo walizianza.

4. Itakapotokea kwamba mwanachama mmoja wa Mahakama atataka kujiuzulu katika Mahakama, maombi ya kujiuzulu yatapelekwa kwa Rais wa Mahakama ili naye ayapeleke kwa Katibu Mkuu. Ufikaji wa maombi hayo kwa Katibu Mkuu utafanya mahali pake huyo mwombaji kuwa pako wazi.

Sehemu ya 14

Nafasi katika Mahakama zitajazwa kwa kufuata njia ile ile iliyowekwa kwa uchaguzi wa mara ya kwanza, lakini kwa kufuata masharti haya yafuatayo: Katibu Mkuu, kati ya muda wa mwezi mmoja toka kutokea nafasi

hiyo, atatoa wito kama ulivyoelezwa katika sehemu ya 5, na tarehe ya uchaguzi itawekwa na Baraza la Usalama.

Sehemu ya 15

Mwanachama wa Mahakama atakayechaguliwa kuchukua nafasi ya mwanachama ambaye muda wake haujesha, mwanachama huyo atashika nafasi hiyo kwa muda ule alioubakisha mwenzake aliyetangulia.

Sehemu ya 16

1. Mwanachama wa Mahakama haruhusiwi kufanya kazi za kisiasa au utawala au kujiingiza katika kazi nyingine ya malipo.

2. Shaka yo yote juu ya jambo hili itasawazishwa kwa uamuzi wa Mahakama.

Sehemu ya 17

1. Hakuna mwanachama wa Mahakama atakayeruhusiwa kuwa ajenti, mshauri au wakili katika kesi yo yote.

2. Hakuna mwanachama atakayeruhusiwa kushiriki katika uamuzi wa kesi yo yote ambayo yeye hapo kwanza alikuwa ajenti, mshauri au wakili wa upande mmojawapo wa wadaawa, au alikuwa ni mwanachama wa mahakama ya taifa ya ulimwengu au wa

tume ya upelelezi au alikuwa na uwezo mwingine wowote.

3. Shaka yo yote juu ya jambo hili itasawazishwa kwa uamuzi wa Mahakama.

Sehemu ya 18

1. Hakuna mwanachama wa Mahakama atakayeweza kufukuzwa ila, kwa kukubaliwa na wanachama wengine wote pamoja, kwamba ameacha kutimiliza masharti yanayotakiwa.

2. Ikiwa ni hivyo, taarifa rasmi itapelekwa na Msajili kwa Katibu Mkuu.

3. Taarifa hii itafanya nafasi ya mwanachama huyo iwe wazi.

Sehemu ya 19

Wanachama wa Mahakama wanapofanya kazi ya Mahakama hiyo ni lazima wapate haki na hifadhi za wajumbe wa kisiasa.

Sehemu ya 20

Kila mwanachama wa Mahakama kabla ya kuanza kazi zake ni lazima ale kiapo mbele ya mahakama kwamba atatumia uwezo wake kwa bidii na bila ya kupendelea.

Sehemu ya 21

1. Mahakama itachagua Rais wake na Makamu wa Rais kwa muda wa miaka mitatu. Nao wanaweza kuchaguliwa tena baada ya muda wao kwisha.

2. Mahakama itamchagua Msajili wake na inaweza kuruhusu kuchaguliwa kwa maafisa wengine kiasi kitakacholazimu.

Sehemu ya 22

1. Makazi ya Mahakama yatakuwa huko Hague. Lakini jambo hili halitazuia Mahakama kukaa na kufanya kazi zake mahali pengine popote itakapofikiria panafaa

2. Rais na Msajili wataishi mahali palipo na Makazi ya Mahakama.

Sehemu ya 23

1. Mahakama itakuwa daima imo kazini isipokuwa wakati wa mapumziko ya kimahakama wakati ambao tarehe zake na muda wenyewe utawekwa na Mahakama.

2. Wanachama wa Mahakama wanayo haki ya kupata siku za likizo. Tarehe na muda wa likizo vitawekwa na Mahakama huku ikiangalia umbali uliopo baina ya Hague na nyumbani kwa kila kadhi.

3. Wanachama wa Mahakama watalazimika siku zote kujiweka chini ya amri ya Mahakama ila iwapo wamo katika likizo au wamezuilika kuhudhuria kwa ajili ya ugonjwa au sababu nyingine ya maana itakayoelezwa kwa Rais.

Sehemu ya 24

1. Ikiwa, kwa sababu fulani maalum, mwanachama wa Mahakama atafikiria kwamba asijiingize katika uamuzi wa kesi fulani, basi atamwarifu hayo Rais.

2. Ikiwa Rais atafikiri kwamba kwa sababu fulani maalum mwanachama mmoja wa Mahakama asiwemo katika kusikiliza kesi fulani, basi atamwarifu hayo mwanachama huyo.

3. Popote itokeapo katika mambo ya namna hii, kuwa Rais na mwanachama hawaafikiani shauri hilo litapatanishwa kwa uamuzi wa Mahakama.

Sehemu ya 25

1. Mahakama kamili itafanya kazi yake isipokuwa kama imeelezwa vingine katika Sheria iliyopo.

2. Kwa kufuata sharti ya kwamba idadi ya makadhi wapatikanao kuweza kutimiza Mahakama isipunguzwe chini ya kumi na moja;

Kanuni za Mahakama zaweza kuruhusu kumkubali kadhi mmoja au zaidi, kwa kufuata hali ilivyo na zamu, asiwepo katika kikao cha Mahakama.

3. Jamii ya kutosha kutimiza Mahakama ni makadhi tisa.

Sehemu ya 26

1. Mahakama yaweza kila baada ya wakati kuweka baraza moja au zaidi litakalokuwa na makadhi watatu au zaidi, kama Mahakama itakavyoamuru, ili kushughulika na namna fulani za kesi, kwa mfano, kesi za wafanyakazi na kesi zinazohusu upelekaji na utumiaji wa habari.

2. Mahakama yaweza wakati wowote kuunda baraza ili lishughulikie kesi fulani. Idadi ya makadhi wa baraza itawekwa na Mahakama pamoja na kukubali kwa wadaawa.

3. Kesi zitasikilizwa na kuamuliwa na mabaraza yaliyoelezwa katika Sehemu hii ikiwa wadaawa watataka hivyo.

Sehemu ya 27

Hukumu itakayotolewa na mabaraza yoyote katika mabaraza yaliyoelezwa katika Sehemu ya 26 na 29 itahesabiwa kuwa imetolewa na Mahakama.

Sehemu ya 28

Mabaraza yaliyoelezwa katika Sehemu za 26 na 29 yaweza, kwa idhini ya wadaawa kukaa na kufanya kazi zake mahali pengine pasipokuwa Hague.

Sehemu ya 29

Kwa kutaka kuharakisha mwendo wa kazi Mahakama itaunda kila mwaka baraza litakalokuwa na makadhi watano, baraza ambalo, kwa maombi ya wadaawa laweza kusikiliza na kukata kesi kwa njia fupi. Zaidi ya hapo makadhi wawili watachaguliwa kwa ajili ya kushika mahali pa makadhi watakaoshindwa kuhudhuria.

Sehemu ya 30

1. Mahakama itatengeneza kanuni za kuendesha kazi zake. Hasa itaweka kanuni za mwenendo wa Mahakama.

2. Kanuni za Mahakama zitaruhusu washauri wa Mahakama kukaa pamoja na Mahakama yenyewe au na baraza lolote la Mahakama, lakini bila ya kuwa na haki ya kupiga kura.

Sehemu ya 31

1, Makadhi wa taifa la kila mdaawa watabaki na haki yao ya kusikiliza kesi itakayokuwa mbele ya Mahakama.

2. Ikiwa Mahakama yachanganya katika makadhi wake, kadhi wa taifa la mmojawapo wa wadaawa, mdaawa mwingine yo yote aweza kuchagua mtu fulani kukaa kama kadhi. Mtu huyo itafaa achaguliwe kutoka katika watu walioteuliwa kuwa ni wagombea uchaguzi kama ilivyoruhusiwa katika Sehemu ya 4 na 5.

3. Ikiwa katika makadhi ya Mahakama hakuna kadhi wa taifa la wadaawa kila mmoja katika wadaawa aweza kuchagua kadhi kama ilivyoruhusiwa katika fasili ya 2 ya Sehemu hii.

4. Masharti ya Sehemu hii yatatumika katika sehemu ya 26 na ya 29. Katika hali kama hiyo Rais anamtaka mmoja au, ikiwa lazima, wawili kati ya wanachama wa Mahakama waliomo katika baraza watowe nafasi kwa wanachama wa Mahakama wa taifa la wadaawa wanaohusika, na kama hawakupatikana au hawawezi kuhudhuria watowe nafasi kwa makadhi maalum waliochaguliwa na wadaawa.

5. Iwapo itatokea kwamba wadaawa mbali mbali watakuwa wanapendelea jambo moja, wadaawa hao, kwa ajili ya masharti yaliyotanguliwa, watatambuliwa kuwa mdaawa mmoja tu. Shaka yo yote juu ya jambo hili itasawazishwa na uamuzi wa Mahakama.

6. Makadhi waliochaguliwa kama ilivyowekwa katika fasili 2, 3 na 4 za Sehemu hii watatimiza

masharti yanayotakikana na Sehemu 2, 17 (fasili 2), 20 na 24 ya Sheria iiyopo. Watashiriki katika uamuzi sawa sawa na wenzao.

Sehemu ya 32

1. Kila mwanachama wa Mahakama atapokea mshahara kwa mwaka.

2. Rais atapokea posho maalum kwa mwaka.

3. Makamu wa Rais atapokea posho maalum kwa kila siku ambayo atafanya kazi ya Rais.

4. Makadhi waliochaguliwa chini ya Sehemu 31, ambao si wanachama wa Mahakama, watapokea fidia kwa kila siku watakayofanya kazi yao.

5. Kiwango cha mishahara hii, posho na fidia kitawekwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Hakiwezi kupunguzwa katika muda wote wa mtu kuwa na cheo fulani.

6. Mshahara wa Msajili utawekwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa kufuata masharti ya Mahakama.

7. Kanuni zitakazotolewa na Baraza Kuu zitaweka masharti ambayo kwayo malipo ya uzeeni yaweza kulipwa wanachama wa Mahakama wa Msajili, na kuweka masharti ambayo kwayo wanachama wa Mahakama na Msajili waweza kurudishiwa gharama zao za safari.

8. Mishahara, posho na fidia zilizotajwa hapo juu hazitalipiwa kodi ya namna yoyote.

Sehemu ya 33

Gharama za Mahakama zitalipwa na Umoja wa Mataifa kwa namna itakavyowekwa na Baraza Kuu.

SURA YA II

UWEZO WA MAHAKAMA

Sehemu ya 34

1. Ni Mataifa tu ndio yanayoweza kuwa ni Wadaawa katika kesi mbele ya Mahakama.

2. Kwa kufuata na kulingana na kanuni zake Mahakama yaweza kukitaka Chama au Shirika la watu la ulimwengu habari yoyote inayohusu kesi zilizo mbele yake, na itapokea habari zilizoletwa na hilo shirika au chama ambazo shirika au chama kimezipata kwa uwezo wake.

3. Iwapo katika kesi mbele ya Mahakama kuna jambo lihusulo maana ya hati ya chama au shirika la ulimwengu au maana ya hati ya mapatano ya ulimwengu yaliyofanywa chini ya hati hiyo, Msajili ataliarifu shirika hilo au chama hicho cha ulimwengu habari hiyo na atalipelekea nakala za mashauri yote ya kesi yaliyoandikwa.

Sehemu ya 35

1. Mahakama itakuwa wazi kwa mataifa ambayo yanashiriki katika Sheria hii iliyopo.

2. Masharti ambayo kwayo Mahakama itakuwa wazi kwa mataifa mengine yatawekwa na Baraza la Usalama kwa mujibu wa masharti maalum yaliyomo katika mkataba uliopo, lakini kwa hali yoyote masharti hayo yasiwafanye wadaawa kutopata usawa mbele ya Mahakama.

3. Iwapo taifa ambalo si mjumbe katika Umoja wa Mataifa ni mdaawa katika kesi Mahakama itaweka kiasi ambacho mdaawa huyo atatoa kwa ajili ya gharama za Mahakama. Sharti hili halitatumika ikiwa taifa lenyewe litachukua sehemu ya gharama ya Mahakama.

Sehemu ya 36

1. Mamlaka ya Mahakama yatachanganya kesi zote ambazo wadaawa watazipeleka na yatachanganya mashauri yote yanayoruhusiwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa au mapatano na maagano ambayo yanatumika.

2. Mataifa ambayo yashiriki katika Sheria iliyopo yaweza wakati wowote kutamka kwamba wanatambua kwa nafsi ya kitendo hicho na bila ya mapatano maalum kuhusu taifa lingine lolote linalokubali lazima hiyo, mamlaka ya Mahakama juu ya kesi zote zinazohusu:

a. tafsiri ya mkataba;
b. jambo lolote la sheria ya ulimwengu:
c. kuwapo kwa tukio lolote ambalo, kama litathibitishwa, lingeleta kuvunjika kwa wajibu wa ulimwengu.
d. umbile na kiasi cha malipo yatakayofanywa kwa ajili ya kuvunjika kwa wajibu wa ulimwengu.

3. Matamko yaliyotajwa hapo juu yaweza kufanywa bila ya sharti au kwa sharti ya kukubaliana kwa mataifa mengi au mataifa fulani tu au kwa wakati fulani tu.

4. Matamko kama hayo yatawekwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ambaye atapeleka nakala za matamko hayo kwa washirika wa Sheria kwa Msajili wa Mahakama.

5. Matamko yaliyofanywa kwa mujibu ya Sehemu ya 36 ya Sheria ya Mahakama wa Kudumu ya Haki za Ulimwengu na ambayo bado yanatumika yatahesabiwa, baina ya washiriki wa Sheria iliyopo, kuwa ni kukubali mamlaka ya lazima ya Mahakama ya Ulimwengu kwa muda wote uliobaki wa kutumika matamko hayo na kwa mujibu wa masharti yake.

6. Itakapotokea ubishi kuwa Mahakama ina mamlaka au haina, ubishi huo utaamuliwa na Mahakama yenyewe.

Sehemu ya 37

Popote mapatano au maagano yaliyopo yaruhusupo kupeleka shauri kwenye baraza iliyowekwa na Ushirika wa Mataifa au kwenye Mahakama ya Kudumu ya Haki ya Ulimwengu, shauri hilo kama ni baina ya washiriki wa sheria iliyopo, litapelekwa kwenye Mahakama ya Ulimwengu.

Sehemu ya 38

1. Mahakama ambayo kazi yake ni kuamua kwa mujibu wa sheria ya ulimwengu, mabishano yanayopelekwa kwenye mahakama hayo, itatumia:

a. Mikataba ya ulimwengu, kama ni ya jumla au mahsusi, yaliyowekwa kanuni zikubaliwazo kwa dhahiri na nchi zinazopongana.
b. desturi ya ulimwengu kuwa ni ushahidi wa matumizi ya kawaida yakubaliwayo kuwa ni sheria;
c. misingi ya kawaida ya sheria itambuliwayo na mataifa yaliyostaraabika;
d. kwa kufuata masharti ya sehemu ya 59, itatumia uamuzi wa kimahakama na mafundisho ya walimu maarufu wa sheria wa mataifa mbali mbali kuwa ni njia ya kuyakinia kanuni za sheria.

2. Sharti hili halitaharibu uwezo wa maha kama wa kuamua kesi kwa kufuata misingi ya maadili na usawa ikiwa wadaawa watakubali hayo.

SURA YA III

MWENENDO

Sehemu ya 39

1. Lugha rasmi za Mahakama zitakuwa ni Kifaransa na Kiingereza. Ikiwa wadaawa watakubaliana kwamba kesi sisikilizwe kwa lugha ya Kifaransa, basi hukumu itatolewa kwa-Kifaransa. Ikiwa wadaawa watakubaliana kwa, mba kesi isikilizwe kwa lugha ya Kiingereza basi hukumu itatolewa kwa Kiingereza.

2. Iwapo hakuna makubaliano ya lugha itakayotumika kila mdaawa katika usemi wake juu ya kesi aweza kutumia lugha atakayopendelea kati ya hizo mbili lakini hukumu itatolewa kwa lugha ya Kifaransa na Kiingereza. Katika hali kama hii, Mahakama wakati huo huo itakata shauri ni ipi katika lugha mbili iwe ni rasmi'

3. Mahakama itakapoombwa na mdaawa itaruhusu lugha nyingine isiokuwa Kifaransa wala Kiingereza itumiwe na mdaawa huyo.

Sehemu ya 40

1. Kesi zitaletwa mbele ya Mahakama, kama itakavyokuwa, ama kwa taarifa ya mapatano maalum ama kwa maombi ya maandishi yatakayopelekwa kwa Msajili. Katika yoyote ya njia mbili hizo ni lazima linalogombaniwa litajwe na wadaawa wanaogombana watajwe.

2. Msajili mara hiyo atapeleka maombi hayo kwa wote wanaohusika.

3. Vile vile atawaarifu Wajumbe wa Umoja wa Mataifa kwa njia ya Katibu Mkuu na pia nchi nyingine yoyote iliyo na haki ya kuhudhuria mbele ya Mahakama.

Sehemu ya 41

1. Mahakama itakuwa na uwezo wa kuonyesha, kama itabidi kufanya hivyo, hatua yoyote ifaayo kuchukuliwa ili kuhifadhi haki ya mdaawa yoyote.

2. Wakati wa kungoja uamuzi wa mwisho, taarifa ya hatua hiyo inayofikiriwa kuchukuliwa mara moja itapelekwa kwa wadaawa na Baraza la Usalama.

Sehemu ya 42

1. Waadawa watasimamiwa na maajenti.

3. Wanaweza kupata msaada wa mshauri au wakili mbele ya Mahakama.

3. Maajenti, mshauri na wakili wa wadaawa mbele ya Mahakama watafaidi haki na hifadhi, iliolazimu ili kuendesha shughuli zao kwa wasaa mwema.

Sehemu ya 43

1. Mwenendo wa Mahakama utakuwa na sehemu mbili: wa maandishi na wa maneno.

2. Mashauri yaliyoandikwa yatachanganya upelekaji wa kumbukumbu, majibu ya kumbukumbu zinazopelekwa Mahakamani na kwa waadawa, na ikilazimu, majibu ya kumbukumbu, vile vile karatasi na hati zinazotia nguvu majibu hayo.

3. Upelekaji huu utafanywa kwa kupitia kwa Msajili kwa taratibu na muda uziozidi ule uliowekwa na Mahakama.

4. Nakala iliyoshuhudiwa ya kila hati iliyotolewa na mdaawa mmoja itapelekwa kwa mdaawa mwingine.

5. Mashauri ya maneno yatachanganya usikilizaji wa Mahakama na mashahidi, mabingwa, maajenti, mshauri na mawakili.

Sehemu ya 44

1. Kwa upelekaji wa taarifa zote juu ya watu wasiokuwa maajenti, na mawakili, mahakama itapeleka moja kwa moja kwa serikali ya nchi ile ambayo nchi yake taarifa hiyo yapelekwa.

2. Njia ya namna hii hii itatumika popote hatua zinapotakiwa kuchukuliwa ili kupata ushahidi wa mahali pale pa matukio.

Sehemu ya 45

Usikilizaji utakuwa chini ya uongozi wa Rais au, ikiwa atashindwa kuwapo basi Makamu wa Rais, na ikiwa wote hawawezi, Kadhi mkubwa ataongoza.

Sehemu ya 46

Kusikilizwa kwa kesi mahakamani kutakuwa hadharani isipokuwa kama Mahakama itaamua vingine, au kama wadaawa watataka watu wasiruhusiwe kusikiliza.

Sehemu ya 47

1. Muhtasari utaandikwa katika kila kikao cha usikilizaji na kutiwa sahihi na Msajili na Rais.

2. Muhtasari huu peke yake utakuwa thabiti.

Sehemu ya 48

Mahakama itatoa amri juu ya namna ya kuendeshwa kwa kesi, na itaamua namna na wakati ambao kila mdaawa ni lazima amalize usemi wake na kuweka mipango yote inayohusu uchukuaji wa ushahidi.

Sehemu ya 49

Mahakama yaweza, ijapokuwa kabla ya kuanza kusikiliza kesi, kuwataka maajenti kutoa hati yoyote au maelezo yoyote. Kukataa kokote kule ni lazima kuandikwe.

Sehemu ya 50

Mahakama yaweza wakati wowote kumpa mtu mmoja, kikundi, ofisi, tume au shirika lolote litakalolichagua, kazi ya kufanya upelelezi au kutoa maoni ya kibingwa.

Sehemu ya 51

Wakati wa kusikiliza kesi swali lolote linalohusika litaulizwa mashahidi na mabingwa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Mahakama katika kanuni za mwendo zilizotajwa katika sehemu ya 30.

Sehemu ya 52

Baada ya Mahakama kupokea uthibitisho na ushahidi ndani ya muda uliowekwa kwa

makusudi hayo, Mahakama yaweza kukataa kupokea ushahidi mwingine wowote zaidi wa maandishi au wa maneno ambao mdaawa atapenda kuutoa isipokuwa kama upande mwingine utakubali.

Sehemu ya 53

1. Popote mmoja wapo wa wadaawa iwapo hakuhudhuria mbele ya Mahakama, au akaacha kutetea kesi yake, mdaawa mwingine aweza kuitaka mahakama ihukumu kwa kufuata madai yake.

2. Mahakama kabla ya kufanya hivyo ni lazima ijitosheleze si tu kwamba ina mamlaka kwa mujibu wa Sehemu ya 36 na 37, bali pia kwamba madai yenyewe yametegemezwa juu ya ukweli na kufuata sheria.

Sehemu ya 54

1. Wakati maajenti, mshauri na mawakili watakapokuwa wamemaliza usemi wao juu ya kesi; Rais, kwa kufuata uongozi wa Mahakama, atatamka kwamba usikilizaji wa kesi hiyo umefungwa.

2. Mahakama itakwenda faragha ili kufikiria hukumu.

3. Mafikirio ya hukumu ya Mahakama yatafanywa faragha na yatabaki siri.

Sehemu ya 55

1. Mambo yote yataamuliwa kwa kufuata uwingi wa makadhi waliopo.

2. Itokeapo kura kuwa sawa sawa Rais au Kadhi aliye mahali pa Rais atakuwa na kura ya kukata shauri.

Sehemu ya 56

1. Hukumu itaeleza sababu zilizotegemezewa hukumu hiyo.

2. Itakuwa na majina ya makadhi walioshiriki katika uamuzi huo.

Sehemu ya 57

Ikiwa hukumu haionyeshi kwa jumla au kwa baadhi umoja wa maoni ya makadhi basi kadhi yo yote atakuwa na haki ya kutoa maoni yake pekee.

Sehemu ya 58

Hukumu itatiwa sahihi na Rais na Msajili. Itasomwa katika mahakama ya hadhara na taarifa ya kutosha iwe imepewa maajenti juu ya kusomwa huko kwa hukumu.

Sehemu ya 59

Uamuzi wa Mahakama hauna nguvu ya kulazimisha isipokuwa baina ya wadaawa na kuhusu kesi hiyo tu.

Sehemu ya 60

Hukumu yenyewe ni ya mwisho na hakuna rufani. Itokeapo ubishani juu ya maana au upeo wa hukumu, mahakama itaeleza maana hiyo kwa maombi ya mdaawa yo yote.

Sehemu ya 61

1. Maombi ya kutaka masahihisho ya hukumu yanaweza kufanywa tu wakati yatakapotegemezwa juu ya ugunduzi wa jambo fulani ambalo namna lilivyo laweza kugeuza hukumu na jambo lenyewe wakati wa hukumu ilipotolewa halikujulikana na Mahakama wala mdaawa anayedai masahihisho hayo, muda wa kuwa kutojua huko hakukusababishwa na kupuuzwa.

2. Kesi ya masahihisho ya hukumu hiyo itafunguliwa kwa hukumu ya Mahakama itakayotajwa wazi kuwepo kwa jambo hili jipya na kutambua kwamba lina sifa ya kuifanya kesi iweze kugeuzwa, na hukumu hiyo itatamka kwamba maombi hayo yakubalike kwa sababu hii.

3. Mahakama yaweza kutaka utimilizaji wa masharti ya hukumu ya nyuma kabla ya kukubali kesi ya mageuzo ya hukumu.

4. Maombi ya masahihisho ya hukumu ni

SURA YA VI

MAONI YA KUSHAURI

Sehemu ya 65

1. Mahakama yaweza kutoa maoni ya kushauri juu ya jambo lolote la sheria kwa maombi ya kikundi chochote ambacho kimeruhusiwa na, au, kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

2. Mambo ambayo kwayo maoni ya kushauri yataombwa mbele ya Mahakama kwa maandishi ni lazima yawe na maelezo kamili ya jambo ambalo latakiwa maoni ya kushauri na yawe na hati zote ambazo huenda zikaweka wazi jambo lenyewe.

Sehemu ya 66

1. Msajili mara moja atatoa taarifa ya maombi hayo ya maoni ya kushauri kwa mataifa yote yapasiwayo na kuhudhuria mbele ya Mahakama.

2. Msajili vile vile ataarifu kwa njia maalum na ya moja kwa moja nchi yoyote inayostahili kuhudhuria au shirika lolote litakalofikiriwa na Mahakama au Rais, iwapo Mahakama haikai, kuwa laweza kutoa habari juu ya shauri hilo, kuarifu kwamba Mahakama iko tayari kupokea usemi wa maandishi, kusikiliza usemi wa mdomo kuhusu jambo hilo mbele ya kikao

cha hadhara, kitakachofanywa kwa ajili hiyo, katika muda maalum utakaowekwa na Rais.

3. Iwapo nchi yoyote inayostahili kuhudhuria mbele ya Mahakama imekosa kupokea taarifa maalum iliyotajwa katika fasili ya 2 ya Sehemu hii, nchi hiyo yaweza kudhihirisha matakwa yake ya kupeleka maelezo ya maandishi au kutaka kusikilizwa; na Mahakama itaamua.

4. Nchi na shirika baada ya kupeleka usemi wake wa maandishi au wa mdomo au yote mawili yataruhusiwa kusema juu ya usemi uliotolewa na madola mengine au shirika nyingine, kwa namna, kiasi na muda maalum ambao Mahakama, au kama Mahakama haikai, Rais ataamua kwa kila kesi fulani. Msajili naye bila kuchelewa atapeleka usemi wowote wa maandishi wa namna hiyo kwenye madola na shirika zilizoleta usemi wa namna hiyo hiyo.

Sehemu ya 67

Mahakama itatoa maoni yake ya kushauri katika kikao cha hadhara baada ya taarifa kutolewa kwa Katibu Mkuu na kwa manaibu wa Wajumbe wa Umoja wa Mataifa na madola mengine na mashirika ya Ulimwengu yanayohusika sana.

Sehemu ya 68

Katika kutimiza kazi zake za kushauri mahakama itazidi kuongozwa na masharti ya Sheria iliyopo ambayo yatumika katika kesi zilizo na magombano kwa kiasi ambacho Mahakama yatambua kwamba inafaa-yafuatwe.

SURA YA V

MABADILISHO

Sehemu ya 69

Mabadilisho kwa Sheria iliyopo yatafanywa kwa kufuata mwenendo ule ule kama unaoruhusiwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa katika kubadilisha Mkataba, lakini kwa kufuata masharti yoyote ambayo Baraza Kuu kwa kupendekezwa na Baraza la Usalama laweza kuyakubali kuhusu kuwamo kwa madola yalio ni wadaawa katika sheria iliyopo ambayo si wajumbe wa Umoja wa Mataifa.

Sehemu ya 70

Mahakama itakuwa na uwezo wa kushauri mabadilisho kwenye Sheria iliyopo kama itakavyoona ni lazima, na itafanya hayo kwa njia ya taarifa ya maandishi itakayopelekwa kwa Katibu Mkuu ili ifikiriwe kwa kulingana na masharti ya sehemu ya 69.

1. Mkutano wa wanachama wa Umoja wa Mataifa, kwa ajili ya kufikiria tena Mkataba wa Umoja huo, unaweza kufanywa mahali popote patakapochaguliwa na tarehe ya mkutano huo, kwa kura za wajumbe wa Baraza Kuu, kwa idadi ya theluthi mbili ya jumla yao, na kwa kura moja ya mjumbe yeyote katika wajumbe tisa wa Halmashauri ya Usalama. Kila mjumbe wa Umoja wa Mataifa atakuwa na haki ya kupiga kura moja tu kwenye mkutano huo.

2. Kukiwa na mabadiliko yoyote yanayotarajiwa kwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa, itabidi kupata uthibitisho wa theluthi mbili za wajumbe wa Umoja wa Mataifa, kuhusu mwenendo wa katiba ya Mkataba huo. Mabadiliko hayo yatapigiwa kura na wajumbe wa Umoja wa Mataifa, kutokana na mapendekezo ya theluthi mbili, za wanachama wa Mkutano Mkuu. Kadhalika wajumbe wote wa kudumu wa Halmashauri ya Usalama itawalazimu kupiga kura juu ya uamuzi utakaopitishwa.

3. Ikiwa Mkutano Mkuu utahitajiwa kufanywa kabla ya kumalizika miaka kumi ya Mkataba uliopo, basi kwanza italazimika Baraza Kuu likutane kutoa kibali cha kuitisha mkutano huo kwa dharura. Theluthi mbili za idadi ya wajumbe wa Baraza Kuu zitahitajiwa kupiga kura kukubali kuitishwa kwa mkutano huo; kadhalika na kura za wajumbe saba wa Halmashauri ya Usalama.